SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 5

**KADA CCM 'amshukia' Polepole**




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Desemba 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580793

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Samia: Hivi ndivyo polisi walivyonitenda

**NI** kabla ya kuwa kiongozi mkubwa, atoa maagizo kwa bosi wao...*Endelea ukurasa wa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan akikagua gwaride la wahitimu wapya wa mafunzo ya uofisa Kozi No. 1/2021 katika mahafali ya kufunga mafunzo ya kozi hiyo, yaliyofanyika katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 3

## RUFANI YA SABAYA KUTAJWA LEO

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, leo inatarajia kutaja kwa mara ya kwanza rufani ya hukumu katika kesi ya jinai...

UKURASA WA 3

## MWANAFUNZI ALIYEJERUHIWA KWA PANGA AFARIKI DUNIA

MWANAFUNZI wa Shule ya Msingi Liganga, Kata ya Mnara, Zulfa Selemani (13) aliyekuwa akitibiwa Hospitali ya Nyangao, mkoani Lindi kwa jeraha la kukatwa panga shingoni na mjomba wake...

UKURASA WA 7

## TANZANIA, MISRI ZATATUA VIKWAZO VYA KODI

TANZANIA na Misri zimekubaliana kuondoa changamoto ya utozaji wa kodi mara mbili kwenye bidhaa...

# CHADEMA yataja vikwazo 3 mkutano wadau wa siasa

UKURASA 3

**RIPOTI MAALUM**

## Madhila waliorejea shuleni baada ya kujifungua

UKURASA 4




Meneja Mipango ya Biashara wa Benki ya CRDB, Masele Msita (wapili kulia), akipokea Tuzo ya Mafanikio ya Ubora kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Jumuiya ya Ulaya ya Utafiti wa Ubora, Edward Ryner, katika hafla iliyofanyika Dubai, Falme za Kiarabu mwishoni mwa wiki. Wengine ambao wameshika cheti ambacho kimeambatana na tuzo hiyo ni Balozi wa Tanzania, Abu Dhabi, Mohamed Abdallah Mtonga (watatu kushoto), Meneja Uhusiano wa Wawekezaji wa CRDB, Anna Mwasha (wapili kushoto) na Meneja Mwandamizi Uwekezaji wa Kijamii wa Biashara, Joycelean Make. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** DABI HAIKUWA RAHISI UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia: Hivi ndivyo polisi walivyonitenda

**Na Elizabeth Zaya**



Rais Samia Suluhu Hassan

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana amefunguka dhidi ya matukio aliyofanyiwa na baadhi ya polisi akiwa kwenye nafasi za chini na raia wa kawaida.

Aidha, amemtaka Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, kufanya maboresho makubwa ili kukomesha rushwa, matumizi ya nguvu bila kutumia akili, kubambikia kesi, kuumiza raia, lugha za kibaguzi, chafu, na dharau.

Rais Samia aliyasema hayo jana wakati wa mahafali ya kufunga mafunzo ya Maofisa Polisi katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Kurasini, jijini Dar es Salaam.

Kuhusu lugha za kibaguzi na chafu alisema: "Kuna lugha ambazo hazipendezi za kibaguzi, kuna siku nilikuwa nimekwenda kwenye harusi ya mkubwa fulani, saa saba usiku narudi nyumbani, nafika njiani taa moja haifanyi kazi, gari moja ya askari ikanifukuza, nikasimama wakaniambia unajua taa yako haifanyi kazi, nikawaambia sijaona, nikashuka kweli nikakuta imeharibika."

"Nikamwambia sawa, niachie asubuhi nitarekebisha, akaniambia hapana sikuachi, mmezidi nyie Waarabu sijui nini akanipa makabila yote, akaniambia lazima nikupeleke polisi, kurudi kilomita 15, nimeingia pale haya mwandikie, sijui wakanong`ona, akaja tena mama njoo eti wewe nani, nikamwambia mimi Samia..."

"Unafanya kazi wapi, nikamwambia nafanya kazi zangu, ulitoka wapi nikamwambia nilishakuambia, akasema basi chukua gari yako uende, sijui katishwa na nani huko, nikamwambia usiku huu niendeshe tena, nikimkuta kama wewe njiani labda unirudishe, ndiyo akanisindikiza kurudi kwangu kama kilomita 10, sasa hii unatumia mabavu badala ya akili."

"Mara nyingine tena nikataka kugongana na gari la polisi, wakanipeleka kituoni, nimefikishwa pale naulizwa na bosi wao, umefanya kosa gani, nikasema kwa kuwa nimefikishwa hapa mimi ndiye mwenye kosa, sasa nitafanyaje, nikawekwa hapo, mpaka Magharibi imeingia na mbu wanauma, naambiwa alaa... mama... hao hawana shamba acha wale tu au tukuingize huko waliko wenyewe (mahabusu), hivi ndiyo lugha zinazotakiwa kuzungumzwa ukiwa kituo cha polisi?"

"Akatoka ofisa, ananiambia uko hapa nikamwambia ndiyo, kuna nini nikamwambia nimetaka kugongana na gari la polisi, gari yenyewe hiyo ilishagongwa ina mashimo kibao, kwa hiyo bosi akauliza hapa umegonga wewe? Nikasema hapana, akauliza kuna mchuno umegonga wewe? Nikajibu hapana. Akawauliza polisi sasa kagonga wapi? Wakajibu hapana alitaka kutugonga. Akawaambia sasa mliwashtaki wapi hawa waliowagonga."

"Nafanyiwa hivyo wakati huo ni mkubwa tu nafanya serikalini, kwa raia wa kawaida hali ikoje?" Alihoji Rais Samia.

**RUSHWA**

"Mara nyingine unasimamishwa njiani na ukimwambia askari polisi ingiza kichwa chako huku tuzungumze, 'can you imagine' (unaweza kuamini), anaingiza kichwa (apokee rushwa) bila kujua ndani ya gari una nondo, una nyundo, hajui chochote anaingiza bichwa lake, unatafuta vijisenti unampa huyo anaondoka, nikamwambia nitakugonga nyundo, mpaka unajiuliza yanatokea haya, labda kwa sababu hatujawapeleka mafunzo au hawajahitimu vizuri mafunzo."

"Tuhuma za rushwa zipo, zinasemwa na nyingine tunaziona kwenye 'clip' za video (video fupi), askari analazimisha mtalii ampatie pesa bila kujua mtalii yule ana kalamu tu inamrekodi kuhusu kile kitendo anachofanya."

Alisema pamoja na kuwa mstari wa mbele kuelimisha namna ya kupambana na rushwa kupitia nyimbo zao, lakini ndio wanalalamikiwa kuongoza kuvikumbatia.

"Ili jeshi litimize kazi zake vizuri, lazima liongozwe na masharti yake au kiapo cha kazi, lakini mara nyingi zana hizi mbili hupuuzwa, na askari kujiona wana nguvu ya ziada na kuacha kufuata misingi ya kazi yake," alisema Rais Samia.

"Kwa bahati mbaya baadhi ya mambo hukiukwa. Kwa mfano kumtisha mtu unapokwenda kumkamata. Tumekuwa tukishuhudia vitisho, ni 'harassment' (unyanyasaji), wakati mwingine mtu anakamatwa tu bila kosa la maana. Umekerana tu na bosi askari basi anaamua kukutia adabu."

**UVUNJIFU WA SHERIA**

Pia, alisema askari wa jeshi hilo, ndiyo wamekuwa mstari wa mbele kuvunja sheria wanazozisimamia.

"Pamoja na kwamba askari ndiyo wasimamizi wa sheria, lakini wengi wenu ndiyo mmekuwa wavunjifu wa sheria hizo, wengine wamekuwa wanatokwa na uaminifu, wanachota mali za watu mali za serikali, vitendo hivyo havijengi jeshi letu," alisema Rais Samia.

Uzembe

Alisema baadhi ya askari wamekuwa wazembe kazini na kutokuyatekeleza ipasavyo majukumu ya kazi zao.

"Unakuta askari yuko lindo, lakini anasinzia kabisaa, unafika pale unaficha silaha au kofia hana habari. Mimi ilishawahi kutokea nilikuta amelala, nikafika nikachukua kofia nikaificha, asubuhi akatafuta, kauliza watoto wote hakuna aliyejua iko wapi, kafika huko sijui kafanywa nini, nikachukua kofia nikampelekea bosi wake nikamwambia ya askari wako alikuwa kalala. Hiyo ni kofia je, ingekuwa silaha," alihoji Rais Samia.

Kadhalika alisema pamoja na vitendo hivyo wanavyofanya, lakini amekuwa akishangaa kuona hata wanapokwenda mafunzo wanafaulu wote.

"Niliwahi kumuuliza IGP kwamba hivi wanaokwenda mafunzo huwa wanashindwa kweli, mbona wengi huwa nawaona wanafaulu, na wengine ukiwaona mh! Sasa unajiuliza wanafaulu vipi wote wakati unapowaambia waingize kichwa kwenye gari ya raia wanaingiza."

Alisema baadhi ya vitendo vya raia kujichukulia sheria mkononi huchangizwa na vitendo hivyo viovu vinavyofanywa na baadhi ya askari.

Aidha, alimtaka IGP kusimamia jeshi hilo lisipate tuhuma mbaya kwa wananchi na kwamba ndiyo mambo yanachangia kushusha imani ya raia kwa jeshi hilo.

Kwa mujibu wa Rais Samia, baadhi ya vitendo vya askari hao kutofuata masharti ya kazi huenda vinachangiwa na masilahi madogo na kuahidi kufanyia kazi.

**ULINZI X-MAS, MWAKA MPYA**

Aliliomba Jeshi la Polisi katika kipindi hiki cha sikukuu kuwa makini na kusimamia vyema kwenye mikusanyiko ya watu wengi kuhakikisha doria zinafanywa mara kwa mara.

Pia alilitaka kuendelea kudhibiti vitendo vya uhalifu kwenye mipaka.

"Vitendo vya uhalifu unaovuka mipaka Kusini mwa Tanzania bado ni mwiba kwa taifa, pamoja na kuvishughulikia, naomba mwongeze nguvu zaidi. Na ni imani yangu kwamba kwa sababu sasa mmepata mafunzo, mtafanyia kazi upungue kwa kiasi kikubwa au uishe kabisa."

Kuhusu ukatili kwa watoto alilitaka jeshi hilo kuendelea kushughulikia na kupambana kupunguza vitendo vya ukatili kwa watoto.

"Ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia na udhalilishaji, ugaidi, biashara za dawa za kulea, biashara haramu ya binadamu, kuzagaa kwa silaha na uhalifu wa kimtandao navyo naomba mwendelee kupambana navyo kuvipunguza au kumaliza kabisa," alisema.

**UPELELEZI KESI**

Alitaka pia kufanyiwa kazi kwa suala la ucheleweshwaji wa upelelezi wa kesi kwa jeshi hilo na kumtaka IGP kuwashughulikia askari wote wenye maadili mabovu, ili kurudisha nidhamu ndani ya jeshi hilo.

**UKUSANYAJI WA SILAHA**

Alilitaka jeshi hilo kuhakikisha linaendelea kufanya ukaguzi wa silaha kwa kuhakikisha zinazobaki ni zile halali na zenye vibali.

Kwa upande wake IGP, Simon Sirro alisema jeshi hilo limekuwa likiwachukulia hatua askari wanaokutwa na utovu wa nidhamu na kwamba wataendelea kufanya hivyo.

"Askari polisi yuko na sare za kazini mbele ya raia, anasifia pombe haramu, sijui na yeye alikuwa tayari kichwani, anasema msiiseme vibaya, sio pombe haramu. Kaipa jina zuri la kimataifa kwamba ni pombe ya kimataifa, angalau utani huo angeufanya akiwa anakula na wenzake, lakini si kwa raia," alionya Sirro.

HABARI KITAIFA

# CHADEMA yataja vikwazo 3 mkutano wadau wa siasa

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema hakitashiriki mkutano wa wadau wa siasa ulioandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Baraza la Vyama vya Siasa nchini, kwa kile walichoeleza ni kukosekana kwa utashi wa kisiasa na uhuru.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema wamepokea barua ya mwaliko wa mkutano huo, lakini msimamo wao ni kutoshiriki kutokana na kupuuzwa kwa mambo matatu waliyotaka yafanyike kabla.

"Katika kikao cha Kamati Kuu ya chama kilichofanyika kidigitali Oktoba 10, mwaka huu, tulijadili hali ya kisiasa pamoja na maazimio mengine tulijadili kuwa vyama viende kushiriki mazungumzo vikiwa huru kufanya shughuli za kisiasa, vyenye kutimiza haki za kisheria na kikatiba ya kisiasa," alisema Mnyika.

Alisema ili kutimiza hayo walitaka mambo matatu kufanyika ambayo ni serikali kutoa tangazo la kusitisha zuio haramu la mikutano ya hadhara na shughuli nyingine za kisiasa kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Pili, ifute kesi zote za kisiasa zilizifunguliwa kabla, wakati na baada ya uchaguzi mkuu, na tatu mashtaka dhidi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe yafutwe ili awe huru kutimiza majukumu yake ya kikatiba ikiwamo kushiriki mkutano wa wadau utakaofanyika Desemba 15, 16 na 17, mwaka huu," alisema.

"Mpaka ninavyozungumza na nyinyi (waandishi) leo (jana) toka tutoe msimamo wa kikao cha uamuzi wa Kamati Kuu hakuna tamko lolote lililotolewa ama na Msajili au Baraza la Vyama vya Siasa au kiongozi mwingine yeyote mwandamizi wa serikali kutangaza kuwa zuio la mikutano ya hadhara na shughuli halali za vyama vya siasa limeondolewa," alisema Mnyika.

Kwa mujibu wa Mnyika, mikutano ya ndani ya chama imekuwa ikiingiliwa na kuvurugwa na Jeshi la Polisi na mingine imekuwa ikiandikiwa barua na jeshi la kuzuiliwa kufanyika kwa sababu za tishio la ugaidi.

Alisema ndani ya miezi miwili tangu watoe rai hiyo, badala ya kesi kupungua zimeongezeka huku akitolea mfano wa kesi mpya iliyofunguliwa Desemba 9, mwaka huu, mjini Buyungu, Wilaya ya Kakonko, waliokamatwa wakifanya kikao cha ndani kwa madai kuwa si halali.

"Uamuzi wa chama Oktoba, mwaka huu wa kutoshiriki mkutano wa wadau wa vyama ulioitwa na Ofisi ya Msajili na Baraza la Vyama vya Siasa upo palepale," alisistiza Mnyika.

# Mwanafunzi aliyejeruhiwa kwa panga afariki

**Na Said Hamdani,** LINDI

MWANAFUNZI wa Shule ya Msingi Liganga, Kata ya Mnara, Zulfa Selemani (13) aliyekuwa akitibiwa Hospitali ya Nyangao, mkoani Lindi kwa jeraha la kukatwa panga shingoni na mjomba wake, Hassani Nguruwe, amefariki dunia. Kwa mujibu wa taarifa iliyothibitishwa na Ofisa Tawala wa hospitali hiyo, Charles Laiser, mwanafunzi huyo alifariki mwanzoni mwa wiki iliyopita.

Zulfa aliyekuwa anasoma darasa la sita Shule ya Msingi Liganga, anadaiwa kujeruhiwa na mjomba wake kwa kukatwa panga shingoni, baada ya wazazi wa mwanafunzi huyo kutaka kumchukua kwa madai mjomba wake kumgeuza mke wa pili wakati akimlea.

Laiser alisema kifo cha Zulfa kimesababishwa na kutokwa damu nyingi na kuchelewa kufikishwa hospitalini kwa matibabu.

Baba wa marehemu, Selemani Juma na Ofisa Mtendaji Kata ya Mnara, Mohamedi Timwanga, walisema kifo cha mwanafunzi huyo kimesikitisha na kuviomba vyombo vya dola kuchukua hatua. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Mtatiro Kitinkwi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo huku taratibu za kubadili mashtaka kwa mtuhumiwa zikiendelea baada ya kifo cha mwanafunzi huyo.

Tukio hilo lilitokea Novemba 15, mwaka huu, baada ya Zulfa kukatwa kwa panga na mjomba wake kwa hasira kutokana na kuchukuliwa na wazazi wake ambao walidai amemgeuza mke wa pili.



Wahitimu wa fani mbalimbali wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) wakila kiapo cha uaminifu katika fani yao wakati wa mahafali ya 19 yaliyofanyika chuoni hapo, Mikocheni jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Rufani ya Lengai Ole Sabaya kutajwa leo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, leo inatarajia kutaja kwa mara ya kwanza rufani ya hukumu katika kesi ya jinai namba 105, iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake wawili.

Ole Sabaya kupitia kwa mawakili wake, walikata rufani Mahakama Kuu, kupinga hukumu iliyotolewa Oktoba 15, mwaka huu na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Odira Amworo.

Mawakili wa Sabaya, akiongozwa na Mosses Mahuna na Fauzia Mustapha, katika rufani hiyo namba 129, waliwasilisha hoja 14 wakiieleza Mahakama Kuu kwa nini hawakuridhishwa na hukumu iliyotolewa awali na Hakimu Odira.

Katika kesi hiyo, mbali na Ole Sabaya washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu na Daniel Mbura, walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha. Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Odira alisema, kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani, imewatia hatiani na kuwahukumu miaka 30 kwenda jela kwa kutenda makosa matatu.

Alisema kosa la kwanza na la pili la unyang'anyi wa makundi pasipo kutumia silaha, Sabaya na wenzake waliwatendea Numan Yasin na Ramadhani Rashi (mashahidi wa Jamhuri), katika duka la Mohamed Saad lililoko Mtaa wa Bondeni, jijini Arusha.

Alisema kosa la tatu ni la unyang'anyi wa kutumia silaha ambalo washtakiwa hao, walimtendea Bakari Msangi, kwa kumpiga, kumfunga pingu, kumtishia silaha na kumpora fedha Sh. 390,000. Alisema hakuna ubishi kwamba Sabaya akiwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, mwenye mamlaka ya uteuzi alitenda makosa hayo kunyume na sheria.

Pia, alisema kwa kuwa mikono yake imefungwa na sheria hawezi kutoa adhabu ya zaidi ya kifungo cha miaka 30 japokuwa wametiwa hatiani kwa makosa matatu na ambayo kila kosa kifungo chake ni miaka 30 na watatumikia adhabu hiyo kwa pamoja.

Alisema kosa la kwanza, la pili na la tatu ni kifungo cha miaka 30 kwa kila kosa na wakati mwingine kifungo kinakwenda sambamba na adhabu ya viboko na kukataa ombi la wakili wa Jamhuri kifungo kuendana na viboko.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, alidai kwamba washtakiwa hao, hawakuwa na kumbukumbu wala rekodi ya kutenda makosa ya jinai ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Alidai kwa kosa la kwanza na la tatu, aliomba mahakama kutoa hukumu ya kuwafunga miaka 30 kwenda jela sambamba na kuchapwa viboko kama sheria inavyoelekeza.

Kadhalika kwa kosa la pili, aliiomba mahakama washtakiwa hao, kuchapwa viboko kwa kuwa ni takwa na kisheria na lipo wazi.

Wakili huyo, alidai kwamba suala la umri kwa washtakiwa halina mantiki, kwa kuwa walipaswa kufanya kazi halali ya kujipatia kipato pasipo kujiingiza katika vitendo vya uhalifu. Baada ya maeleza hayo, kutoka kwa wakili wa Jamhuri, Wakili wa mshtakiwa wa kwanza (Sabaya), Mosses Mahuna, alidai ni kweli kuwa sheria imeeleza wazi ukitiwa hatiani kifungo ni miaka 30 na kinaweza kuambatana na viboko au visiwepo kabisa.

"Tunaomba umwonee huruma mshtakiwa wa kwanza hili ni kosa lake la kwanza, alikuwa mtumishi wa serikali na amelitumikia taifa hili, hivyo tunaomba mahakama kutoa adhabu ambayo imeangalia vizuri kwa kutambua huduma alizotoa katika jamii," alidai Mahuna.

Ailieleza mahakama hiyo kwamba, kwa kuwa mshtakiwa alitoa ushirikiano kwa vyombo vya dola alipokamatwa, pia bado ni kijana mdogo na ni nguvu kazi ya taifa, endapo atafungwa kifungo cha miaka mingi maisha yake yataishia gerezani na kuomba kupewa adhabu ambayo muda sio mrefu atarejea tena uraiani kuendelea na majukumu mengine ya kijamii.

"Familia, mke na watoto wanamtegemea tunaomba adhabu iwe kwa pamoja kwa makosa yote, kwa kuwa adhabu ikiwa kwa kila kosa atafungwa miaka 90 na sasa hivi tayari ana miaka 34, hivyo atatoka gerezani akiwa na miaka 124, tunaomba ikiwezekana iwe miaka 30 tu," aliomba Mahuna.

RIPOTI MAALUM

# Madhila yaliyoko waliorejea shuleni baada ya kujifungua

## ■Likizo ya corona yatajwa tatizo

**Na Elizabeth Zaya,** MPWAPWA

"TUNATAMANI na sisi tusome kama ilivyo kwa wenzetu walioko katika mfumo rasmi wa elimu ili tutimize ndoto zetu ambazo zilikuwa zimeanza kufifia," Anty Rafaeli, mwanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi kilichoko Kijiji cha Kisale, Mpwapwa, anapaza sauti kuhusu kinachojiri chuoni kwao.

Anty ni miongoni mwa wasichana waliopata fursa ya kuingia katika mpango unaoitwa 'Elimu Haina Mwisho', ambao serikali inaufadhili kwa kuwarudisha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo yao katika mfumo rasmi wa elimu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito.

"Tunashukuru serikali kutusaidia katika kutuletea programu hii, lakini ni vizuri kabla ya kuianzisha ilitakiwa iwe imetukamilishia kila kitu ambacho kinahitajika shuleni, tofauti na ilivyo sasa, bado kuna vitu vingi havijakaa sawa," anabainisha dosari anazoziona katika mfumo huo wa elimu.

Anty anakumbusha kuwa alikatisha masomo baada ya kupata ujauzito akiwa kidato cha tatu mwaka 2018 katika Shule ya Sekondari Ikuya wilayani Mpwapwa, akinyoshea kidole kuachana kwa wazazi wake kuwa kiini cha tatizo.

Anasema kuwa baada ya kuachana kwa wazazi, aligeuka kuwa mlezi wa wadogo zake na hivyo kujikuta akiingia kwenye uhusiano wa kimapenzi ili kupata fedha kwa ajili ya kuendesha familia.

Anty anakumbusha kuwa kabla ya kufukuzwa shuleni, alikuwa anachukua masomo sayansi na malengo yake makubwa yalikuwa ni kuwa daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake na watoto na alikuwa anafanya vizuri darasani.

"Nilipofukuzwa shule nilipoteza mwelekeo, sikuamini kile kilichonitokea, kwamba ndoto yangu ndio imeishia pale na hata mtu aliyenipatia ujauzito alinikimbia.

"Mwaka jana walipotangaza kwamba serikali imeleta programu hii, kijijini kwetu nilikuwa wa kwanza kujiandikisha, niliona kama muujiza kwangu na nikaanza kuona kama ninaenda kufufua ndoto yangu iliyokuwa imezima.

"Nilichaguliwa kujiunga katika chuo hiki na mtoto wangu ikabidi nimpeleke kwa mama yangu, kwa sababu sisi tuliambiwa tutakuwa tunaishi hukuhuku chuoni.

"Niseme tu ndani ya moyo wangu, niliishukuru sana serikali kwa hili. Lakini moyo wangu ulipatwa na huzuni baada ya kufika hapa na kukuta hakuna walimu wa kufundisha masomo ya sayansi.

"Niliumia kwa sababu ndoto yangu tangu awali ni kusoma masomo hayo ili baadaye niwe daktari bingwa, hii ndiyo ndoto yangu kubwa, lakini nimelazimika kuchukua masomo ya sanaa kwa sababu 'ndo' yenye walimu hapa chuoni.

"Kwa hiyo imenibidi nisome kitu ambacho sikukipenda na sikukitarajia, lakini kwa sababu siwezi kuacha kutumia fursa hii na lengo langu ni kutaka kusoma nifike mbele, itabidi nijitahidi nifanye vizuri niendelee mbele na nisome sheria nije kuwa wakili nisaidie nchi yangu na makundi mbalimbali katika masuala ya kisheria na namna ya kupata haki zao," Anty anasimulia.

Alitoa rai kwa serikali ihakikishe masomo yote ya sanaa na sayansi yanafundishwa katika chuo hicho na vingine vya hadhi huyo, pia madarasa, mabweni na kila kitu kinachohitajika.



Baadhi ya wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Mpwapwa wakiwa darasani, hawa ni waliorejeshwa shuleni kwa mpango maalum wa serikali baada ya kukatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito.
**PICHA: ELIZABETH ZAYA**

### MKASA ULEULE

Lucy Denye, mwanafunzi mwingine chuoni huko mwenye historia na mkasa unaofanana na mtangulizi wake Anty, anasema alikuwa na ndoto ya kuchukua masomo ya sayansi lakini amelazimika kusoma masomo ya sanaa kwa kuwa chuo hakina walimu wa sayansi.

Lucy anasimulia kuwa alikatisha shule kutokana na kupata ujauzito akiwa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Namweta wilayani Mpwapwa.

"Sina namna, imebidi nisome masomo ya arts (sanaa) kwa sababu walimu wa sayansi hawapo, japo halikuwa kusudio langu," Lucy analalama.

Anasema licha ya serikali kuwasaidia kupitia programu hiyo, bado mazingira siyo wezeshi kwa kuwa baadhi ya vitu havijakamilika ikiwamo upungufu wa walimu, madarasa, vitabu na maabara.

"Kama serikali ilikuwa inataka tusome katika mazingira mazuri kama wanafunzi wengine, ingekamilisha kila kitu lakini si kama ilivyo kwa sasa, mazingira ni magumu sana, tunasoma 'kiugumuugumu', darasa lenyewe tunalotumia sisi ni lile la wanafunzi wanaosoma ufundi uashi, la kwetu hatuna.

"Walimu wanaokuja kutufundisha wapo wawili tu, hatuna maabara wala hakuna vitabu, yaani mazingira bado hayajawekwa vizuri," Lucy anafafanua madhila ya mfumo huo wa elimu.

### MKUU AKIRI

Mkuu wa chuo hicho, Lucy Paul, anakiri kuwapo dosari zinazonyoshewa vidole na wanafunzi wake, akibainisha kuwa programu hiyo ya serikali inahitaji maboresho zaidi.

Anasema mpaka sasa walimu waliopo ni wawili wakati uhitaji ni walau kuwa na walimu wanne kwa ajili ya programu hiyo.

"Na hao wanalazimika kufundisha masomo ambayo siyo yao kwa sababu hakuna wengine, kwa kweli bado tuna uhitaji mkubwa wa walimu, lakini hata madarasa yao ya kusomea hakuna na hata mabweni.

"Wanafunzi walioko katika programu hii tulionao hapa wengi ndio hao waliokatisha masomo kwa ujauzito. Kwa hiyo kulitakiwa kuwe na darasa la kulelea watoto wao na kwa sababu halipo inabidi wawaache nyumbani. Kwa ujumla, bado tuna uhitaji wa kuboreshewa miundombinu kwa ujumla wake pamoja na walimu," anasema.

Kiongozi huyo wa chuo anabainisha kuwa walianza kusajili wanafunzi kupitia programu hiyo ya 'Elimu Haina Mwisho' Februari mwaka jana, wanafunzi 47 wakisajiliwa, lakini walipokwenda likizo baada ya mlipuko wa virusi vya corona, wanafunzi 19 tu wairejea kuendelea na masomo.

"Kati ya hao 19 waliorejea baada ya likizo ya corona, 18 wamefanya mtihani wa kidato cha pili (QT) na mmoja amefanya mtihani wa kidato cha nne.

"Bado hakuna mwitikio wa wananchi kutumia vyuo hivi licha ya kwamba programu hii ya 'Elimu Haina Mwisho' inaendeshwa bila malipo kwa wanafunzi hao," anabainisha.

### KAULI YA WAZAZI

Shekifu Ally, mkazi wa Mpwapwa na mmoja wa wazazi waliopeleka watoto katika chuo hicho, anabainisha kuwa amelazimika kumtoa binti yake katika chuo hicho baada ya kuelezwa upungufu uliopo.

Anasema kwa sasa binti yake anasoma mjini Dodoma, akifafanua: "Mwanangu aliacha masomo akiwa kidato cha kwanza baada ya kupata ujauzito. Mwaka jana niliposikia serikali imeleta hiyo programu, nikampeleka kwenye chuo hicho.

"Alipofika huko (chuoni) akaniambia kwamba masomo anayotaka kusoma hakuna. Alisoma mwezi mmoja tu, walivyorudishwa kwa ajili ya corona alikataa kabisa kurudi, akasema anataka kusoma sayansi. Ilibidi niuze shamba langu, nikampeleka huko Dodoma mjini, anasoma QT," anasema.

### OFISA MAENDELEO

Kaimu Ofisa Maendeleo ya Jamii wilayani Mpwapwa, Abdu Mangapi, anakiri bado kuna uhitaji mkubwa wa kuboresha miundombinu katika chuo hicho cha maendeleo ya wananchi pamoja na kuendelea kuhamasisha wananchi kukitumia.

"Ni kweli bado miundombinu katika chuo hicho siyo ya kuridhisha, bado tunaendelea kuomba kwa serikali kuu kuongeza bajeti ya kuboresha, lengo kiwe na kila kitu na kutumiza lengo lililokusudiwa," anasema Mangapi.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ilianzisha programu ya Elimu Haina Mwisho (EHM) kwenye vyuo vya maendeleo ya wananchi (FDC) ambao ulilenga kuwasaidia wasichana wenye umri usiozidi miaka 25 waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwamo ujauzito.

Takwimu za Elimu (BEST 2020) mwaka 2015, zinabainisha kuwa wanafunzi wa kike 3,439 waliacha shule kwa sababu za ujauzito na idadi hiyo iliongezeka hadi kufikia wanafunzi 6,533 mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 90.

HABARI KITAIFA

# CCM kidedea uchaguzi Ngorongoro

**Na Mwandishi Wetu**

MGOMBEA Ubunge Jimbo la Ngorongoro kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Emmanuel Shangai, ametangazwa mshindi kwa kupata kura 62,017 kati ya kura halali 62,461 kwenye uchaguzi mdogo wa jimbo hilo uliofanyika Desemba 11, mwaka huu.

Msimamizi wa uchaguzi huo, Dk. Jumaa Mhina, alimtangaza Shangai kuwa mshindi baada ya majumuisho ya kura zote kutoka kwenye vituo mbalimbali.

Wagombea wengine wa vyama 11 vilivyoshiriki uchaguzi huo na kura zao kwenye mabano ni Chama cha ACT-Wazalendo, Johnson Gagu (170), Saimin Paul Ngilisho wa Chama cha Demokrasia Makini (105), Mohamed Kitundu wa Chama cha ADC (63) na mgombea wa Chama cha ADA TADEA Mwinyi Hamisi (30).

Wengine ni Mary Daud wa UPDP (20), Juma Feruziyson wa NRA na Amina Amir Mcheka wa NLD (16) kila mmoja.

Mwita Makuru wa Chama cha UDP (10), Saimon Johnson wa SAU (9) na Frida Marko Nko wa UMD (5).

Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Jimbo la Ngorongoro umefanyika baada ya aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo,

# Bulembo 'amshukia' Polepole

**Na Gwamaka Alipipi**

KADA wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Abdallah Bulembo, amemwomba Makamu Mwenyekiti CCM Bara, Philip Mangula, vikao vya juu vya chama hicho kumhoji na kumchukulia hatua mbunge wa kuteuliwa, Humphrey Polepole, kwa kile alichodai kumkosea heshima Rais Samia Suluhu Hassan.

Amesema Polepole amekuwa akimwingilia kiutendaji Mwenyekiti wa CCM ambaye ni Rais wa nchi, kitendo ambacho ni kinyume na taratibu za chama hicho na kwamba anapaswa kuhojiwa na kuchukuliwa hatua kali ikiwamo kufukuzwa uanachama.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari, pamoja na mambo mengine alishangaa viongozi wa ngazi za juu CCM kutomchukulia hatua mbunge huyo wa kuteuliwa kutokana na kauli zake tata anazozitoa mara kwa mara.

Hivi karibuni Polepole alinukuliwa na vyombo vya habari akieleza kuwa alitamani Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Hayati John Magufuli, ingemaliza watu aliowaita wahuni, ambayo haikuwamaliza wote, kauli iliyozua mjadala.

Pia, juzi akizungumza na waandishi wa habari alieleza kuwa wahuni ni watu wanaotanguliza maslahi yao mbele badala ya maslahi mapana ya taifa.

Kadhalika, aliwahi kunukuliwa na vyombo vya habari akieleza kupinga ujio wa chanjo ya virusi vya corona nchini pamoja na zoezi la kuchanja.

Bulembo akizungumza na waandishi alisema ndani ya CCM mwanachama anapokwenda ndivyo sivyo na misingi ya chama huitwa katika vikao vya chama na kupewa onyo ama adhabu ya kusimamishwa au kufukuzwa, lakini alidai kwa Polepole imekuwa kimya kirefu.

"Nimeanza kumfahamu Polepole mwaka 2012 wakati akiwa katika timu ya wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, mimi nilikuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu CCM, tulikuwa tunabishana mambo ya serikali tatu. Ni mtu mdogo sana ndani ya chama, lakini anapata kiburi cha kumkwamisha Rais Samia kufanya kazi," alisema Bulembo na kuongeza:

"Hivi Mzee Mangula yupo? Yeye ni nani (Polepole) hadi anaogopwa. Polepole hamjali wala hamuheshimu Rais Samia Suluhu Hassan. CCM tunaheshimiana, mkuu akisema wengine tunatii sasa kwa nini yeye anakiuka?" alihoji Bulembo.

Bulembo ambaye aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM, alisema kama Polepole ana jambo analotaka kulitimiza ni vyema akaondoka ndani ya CCM na kulitekeleza akiwa nje ya chama.

"Aliwahi kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Musoma, aliteuliwa kuwa Katibu wa Itikadi na Uenezi wa chama, kutoka uraiani hadi kuwa Katibu Mwenezi wa chama mtu ambaye hajawaji kuwa hata chipukizi wa chama, hajawahi kugombea nafasi yoyote ndani ya chama, tulikubali kwa sababu aliyemteua ni mwenyekiti wetu, tulitii mamlaka, sasa yeye leo hataki kutii mamlaka kwanini?" Alihoji.

Kadhalika, Bulembo alisema Polepole anafanya mambo hayo kwa sababu hajui misingi ya CCM kunakosababishwa na kutopitia nafasi mbalimbali ngazi ya chini za chama ikiwamo UVCCM, chipukizi, ambazo zinamjenga mwanaCCM kimaadili.

"Mimi naamini kuna watu wako nyuma ya Humphrey Polepole kwa haya anayoyafanya ambao wanamtuma na kumuunga mkono. Ila ninachotaka kusema hawatusumbui, CCM imesimama katika misingi ya maadili, ilikuwapo na itaendelea kuwapo," alisisitiza.

Aliwasihi wananchi kumuunga mkono Rais Samia Hassan kwa kile anachokifanya kwa sababu anaijenga Tanzania kiuchumi na kuitangaza kimataifa kupitia hotuba anazozitoa kwenye mikutano.



Meneja wa Maabara ya Sayansi Jinai ya Kemia, Elias Mulima (kulia) wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali akitoa mafunzo ya usimamizi wa sampuli za jinai kwa askari wa Jeshi la Polisi, yaliyofanyika Chuo cha Polisi Kidatu mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGA WETU**

# Utouh abaini tatizo wanafunzi wa vyuo vikuu

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, amesema kuna ukosefu wa elimu ya uwajibikaji kwa baadhi ya wanafunzi wa vyuo vikuu, hali inayowafanya kutojua umuhimu wa kushiriki katika upangaji wa bajeti ya serikali.

Utouh, aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka minane kuanzia mwaka 2006, alibainisha hayo juzi alipokutana na baadhi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Taasisi hiyo ilikuwa imeandaa mjadala wa pamoja na wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu ushiriki wa vijana katika mchakato wa uandaaji bajeti.

Alisema dhumuni la WAJIBU kuandaa mjadala huo na kuzuru chuoni huko ni kutoa elimu na kuwahamisha vijana kuacha kukaa na kulalamika, badala yake wajihusishe na upangaji wa bajeti za serikali kuanzia ngazi ya serikali za mtaa hadi serikali kuu.

"Tumekuja kukutana na vijana ikiwa ni moja ya shughuli za WAJIBU kutoa elimu kwa vijana juu ya ushiriki wao katika kuandaa bajeti.

"Kama vijana wakielewa kuwa fedha zinazotumika kuendesha maendeleo ni fedha za wananchi, ni dhahiri kwamba watapata uchungu pale zitakapokuwa zinatumika kinyume cha utaratibu.

"Tunajua vijana wakielewa madhara ya rushwa kwa jamii, itasaidia kuongeza nguvu kazi katika kupambana na rushwa," alisema.

Utouh alibainisha kuwa katika utoaji wa elimu hiyo, tayari taasisi hiyo imeshawafikia vijana 12,000 na wanaamini vijana hao watakuwa mabolozi wazuri wa kusambaza elimu hiyo.

"Ninaamini baada ya muda tutakuwa na jeshi kubwa ambalo linaamini rushwa ni adui wa haki na wataamini kuwa pesa za serikali zinapohujumiwa tunaoumia ni sisi watu wa chini," Utouh alisema.

Aliwataka wanafunzi wa UDSM, hususani wanaochukua masomo ya biashara, kununua na kukisoma kitabu alichokiandika na kukitoa hivi karibuni, ambacho alidai kitawaongezea ujuzi katika fani zao.

"Nimeandika kitabu, nimekipa jina la 'Principles of Public Sector Auditing, The Case of Sai Tanzania. Kitabu hiki kilizinduliwa juzi na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba. Kimsingi kitabu hiki kinazungumzia zaidi misingi ya ukaguzi katika sekta ya umma," alisema.

Mwakilishi wa Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. Lazaki Lokina, alisema uwajibikaji ni nyenzo muhimu katika kupambana na rushwa na kuahidi kuundwa kwa klabu ya uwajibikaji chuoni huko ili kufanya wanavyuo kuendelea kukumbatia elimu hiyo.

"Niseme tu tunalishukuru Taasisi ya WAJIBU kwa kukitembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hakika leo (juzi) wamekuja na mada ambazo ni muhimu kwa taifa letu.

"Ni ukweli usiopingika vijana ndio nguvu kazi ya taifa na rushwa huwa inatawala pale uwajibikaji unapopungua. Uwajibikaji ni nyenzo muhimu katika kupambana na rushwa.

"Niwatake wanafunzi mliohudhuria huu mjadala mkawe macho katika kuchangamkia fursa ya upangaji wa bajeti ili kupata nafasi ya kuchangia hoja kwa serikali zitakazokuja na mitazamo chanya kwa jamii," alisema.

Mhadhiri na Mkuu wa Idara na Utafiti na Ushauri katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Jonas Kapwani, alisema ili bajeti ya serikali ikamilike lazima kuwe na malengo na shabaha ambayo kwa kiasi kikubwa inatakiwa kuchangiwa na vijana. Ofisa Mchunguzi Mkuu Mkoa wa Kinondoni wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU), Dorothea Mrema, aliwataka wanafunzi wa chuo hicho kutojihusisha na vitendo vyovyote vinavyoashiria rushwa.

"Rushwa ni adui wa maendeleo na haki pia rushwa yoyote, hata ikiwa rushwa ya ngono, ni adui wa haki. Kama ukikumbana na mazingira yanayoashiria rushwa ya ngono pigeni simu 113 bure na hapohapo TAKUKURU watachukua hatua," alisema.

Mwanafunzi wa mwaka wa tatu katika chuo hicho anayechukua kazo ya elimu, Jane Limwata, alishukuru Taasisi ya WAJIBU kwa kuwaongezea uelewa mkubwa kwa vijana, hususan kuhusu ushiriki katika upangaji wa bajeti ya serikali.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ligi Kuu inahitaji wadhamini zaidi, ila kwa hili TFF ichutame

LIGI Kuu Tanzania Bara ambayo msimu huu inashirikisha jumla ya timu 16, imekuwa na ushindani mkubwa tofauti na misimu mingi iliyopita, hii ikichangiwa na dau kubwa lililowekwa na wadhamini wa ligi hiyo kwa upande wa haki za matangazo ya televisheni, Azama Media Ltd.

Kwa mujibu wa mkataba huo wa Sh. bilioni 225. 6, kwa kipindi cha miaka 10, kwa msimu huu bingwa atapata Sh. milioni 500 mshindi wa pili Sh. milioni 250 wa tatu Sh. milioni 225 wa nne Sh. milioni 200 na dau hilo litashuka likipungua hadi timu itakayoburuza mkia pia itapata kiasi chake.

Si kiasi hicho pekee ambacho kimeongeza ushindani, kwani uwapo wa dau la Sh. bilioni 2.5 (kabla ya VAT) kutoka kwa mdhamini mkuu, Benki ya NBC iliyoingia mkataba wa miaka mitatu na lile la Sh. bilioni 3.54 kwa kipindi cha miaka 10 kutoka Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kwa upande wa matangazo ya redio, yamechangia pia.

Hii inadhihirisha kwamba ongezeko la wadhamini linafanya ushindani kuongezeka na kuipa thamani zaidi ligi yetu ambayo inashika nafasi ya nane kwa ubora barani Afrika. Hivyo, tutakuwa wachoyo wafadhila kama hatutatoa kongole kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) pamoja na Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), kwa juhudi na kazi kubwa waliyoifanya na wanayoifanya kushawishi wadhamini kuidhamini ligi yetu. Pamoja na kongole hizo, upo msemo usemao "mkubwa akivuliwa nguo huchutama", ndivyo inavyotakiwa kwa TFF kufanya kwa sasa baada ya Klabu ya Simba kutoa malalamiko kuhusu mkataba mpya wa shirikisho hilo na Kampuni ya GSM.

GSM ambao ni wadhamini wakuu wa Klabu ya Yanga, lakini ikiidhamini Namungo FC na Coastal Union, imeingia mkataba na TFF kuwa mdhamini mwenza wa ligi hiyo kwa masharti kwamba nembo yao ikae kushoto mwa bega la jezi za timu zote 16 za Ligi Kuu.

Hata hivyo, kwa madai ya Simba hakuna klabu iliyoshirikishwa zaidi ya kuona picha kupitia mitandao ya kijamii ikionyesha viongozi wengi wa Yanga na wale wa TPLB waliohudhuria siku ya kusainiwa mkataba huo.

Hivyo, Simba inadai kutakuwa na mwingiliano wa kimaslahi hasa kwa kuzingatia kanuni ya 16 ya udhamini ambayo inakataza moja kwa moja klabu kuingia mkataba na wadhamini wa TFF na kuzikataza kufanya mawasiliano yoyote ya moja kwa moja na wadhamini wa shirikisho hilo.

Lakini kanuni hiyo inatamka wazi mdhamini mkuu wa ligi hiyo ndiye anayepaswa kukaa katika bega la kulia la jezi za timu zote shiriki na hakuna sehemu anatajwa mdhamini mwenza, hivyo kuona kuna ukiukwaji wa kanuni kwa TFF kuzilazimisha kuvaa logo ya GSM kushoto. xAwali, baada ya kusainiwa kwa mkataba huo, kuliibuka minong'ono mingi, lakini TFF ilitoa taarifa na kueleza mkataba huo ni wao na GSM, hivyo hakuna anayepaswa kuhoji, lakini siku tatu kabla ya mechi ya watani wa jadi iliyopigwa juzi, ndipo mtafaruku ukatokea baada ya agizo kutoka TPLB kuitaka Simba na klabu zote kuanza kutumia logo ya kampuni hiyo.

Simba kama zilivyo klabu zingine licha ya kutojitokeza hadharani, zinadai zilipaswa kushirikishwa na kama GSM anahitaji kutangazwa kupitia jezi zao, basi waketi mezani, lakini si kupitia kwa udhamini wa TFF kinyume cha kanuni ya 16 ya udhamini.

Yapo mengi ya msingi ambayo Simba inaonekana kuwa na hoja hasa kwa kusimamia kanuni, hivyo cha muhimu ni TFF kukubali kuchutama baada ya kuvuliwa nguo ili kuzilinda kanuni walizojiwekea badala ya kupandisha mabega juu, kwani kwa hilo itakuwa inazinyima haki klabu kuwa na uhuru wa kujitafutia wadhamini wao kupitia jezi zao hasa kwa kuzingatia zipo ambazo tayari zina wadhaminiwa wao katika bega lao la kushoto.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Barbara kuzuiwa kuingia uwanjani ni kukimbiza wanawake kwenye soka

Na Adam Fungamwango

**WAKATI** inakaribia tu kuanza mechi ya Simba na Yanga, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, aliandika kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram kuwa amezuiliwa kuingia uwanjani kutazama mechi hiyo.

"Asante sana Bodi ya Ligi kwa kunizuia kuingia kwenye mechi na familia yangu, Mungu Ibariki Simba," aliandika Ofisa Mtendaji Mkuu huyo. Alisema alikwenda na watoto wake wawili na ndugu yake mmoja ambao wote walikuwa na kadi za kuingilia, lakini walimkatalia katakata kuingia.

"Wakati nazuiliwa kuingia uwanjani CEO wa Bodi ya Ligi alikuwapo na aliniona, lakini alinipita bila kusema chochote. Wamenikosea sana heshima. Haikubaliki," alisema Barbara.

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, wakati mechi ikiendelea, Shirikisho la Soka nchini (TFF) likatoa taarifa yake, kitu ambacho si cha kawaida sana. Ilikuwa ni haraka mno kujibu shutuma za Barbara.

TFF, pamoja na mengine yanayohusiana na tukio hilo, iliandika kusikitishwa na vitendo vya vurugu vilivyofanywa na baadhi ya viongozi wa Simba kwenye eneo la kuingilia Jukwaa la Watu Maalum (VVIP), Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi hiyo. Ikadai Ofisa Mtendaji Mkuu huyo wa Simba alifika katika eneo hilo akiwa ameongozana na watoto watatu ambao hawaruhusiwi kuingia katika eneo hilo na walikuwa na kadi za watu wengine waliolikwa kinyume cha utaratibu unavyotakiwa, huku Barbara yeye akiruhusiwa kuingia, lakini eti alianza kutoa lugha isiyofaa huku akirekodi tukio na baadaye kutupa kadi na kuondoka.

Ukiangalia sakata hili, linaonyesha kabisa wala halikutakiwa kuwapo. Kuna busara fulani na utamaduni wa Kitanzania ambao ilibidi ufuatwe ili kulimaliza.

Hata askari wetu wa Jeshi la Polisi, pamoja na kwamba wanasisitiza sheria bila shuruti, lakini tunaona kuna maeneo au kuna wakati wanatumia busara na utamaduni wetu ili kumaliza tatizo linalojitokeza kwa ajili ya kuondoa mzozo au tatizo lisilo la lazima.

Ilishindikana vipi kusulushisha jambo dogo kama hili? Ndiyo maana pamoja na Barbara na watoto wake kukataliwa, lakini kwenye eneo hilo hilo la VVIP kulikuwa na watoto wengi tu. Je, hao walikuwa na kadi halisi za mialiko? Ilivyozoeleka hata kwenye harusi au sherehe mbalimbali, kadi hata iandikwe jina, kama mwenyewe ameamua kumpa mtu mwingine aende au amwakilishe anaruhusiwa. Kama zilikuwa za viongozi wa Simba ambao hawakuja, kulikuwa na ubaya gani watoto hao kuchukua nafasi zao? Halafu nasikia pia kuna kiongozi mwingine wa Simba alizuiliwa. Hapa ndipo tutaanza kuona huenda kuna kitu nyuma ya pazia.

Unajiuliza, hivi Barbara ni mara ya kwanza kwenda uwanjani na watoto? Na kama alikuwa anakwenda nao mbona hawajawahi kuzuiwa? Hivi hajui taratibu? Kwani ni mara yake ya kwanza kwenda viwanjani? Mbona hatujawahi kuona amezuiwa? Barbara huyu huyu mbona huwa anasafiri na klabu yake Simba nje ya nchi, pamoja na fitina zote za mechi za kimataifa, hatujasikia amezuiwa?

Au hii ni mechi ya kwanza kwa Barbara kuingia zikicheza Simba na Yanga? Na kama kuna kiongozi mwingine wa Simba alizuiliwa na baadaye aliingia, kwa nini naye alizuiliwa? Na kwa nini waliozuiliwa wote ni wa Simba? Na kwa nini zisiwe siku tofauti ni siku hiyo hiyo moja tu?

Haya ni maswali ya kiintelijensia. Huwa wanajiuliza watu wanaintelijensia, ambao wataangalia tukio lolote kwa jicho la tatu na siyo yale mawili ambayo wote wanaangalia.

Hata kama inawezekana siyo, lakini moja kwa moja hili litahusishwa na sakata la viongozi wa Simba kupinga udhamini wa mmoja wa wadhamini wenza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa sababu Barbara na baadhi ya viongozi wa Simba walikuwa mstari wa mbele kuhakikisha timu ya Simba haivai nembo ya mdhamini, lakini hata mabango hawayataki. Yaliondolewa siku moja kabla ya mechi. Wanaoangalia mambo kwa jicho la tatu, wanaamini kuwa huenda tatizo limeanzia hapo, kwa hiyo kinachoendelea ni kutunishiana misuli, au kulipiana visasi na kutafuta namna ya kuadhibiana kwa faini zisizo za msingi.

Hivi sasa wanawake wamekuwa wakiingia kwenye uongozi maeneo mbalimbali na wameonekana kuwa viongozi bora kwa muda mfupi tu kwenye nyanja mbalimbali. Baadhi yao ni kwenye michezo ambako Barbara amekuwa mfano, kwani huko nyuma wanawake waliogopa sana kujihusisha kwenye michezo kwa kile kilichoonekana kuwa ni mambo ya 'kihuni'.

HABARI KITAIFA

# 'Morocco Square' kukamilika Juni mwakani

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Mkandarasi wa Kampuni ya Ujenzi ya Estim Construction kuhakikisha mradi wa ujenzi wa 'Morocco Square', unakamilika kufikia Juni 30, 2022.

Kauli hiyo ya Dk. Mabula inatokana na serikali kuliruhusu shirika hilo kukopa fedha kwa ajili ya kumaliza mradi huo uliokuwa umesimama kwa takriban miaka mitatu sasa.

Kwa mujibu wa Msimamizi wa mradi huo kutoka NHC, Samuel Metili, mradi wa Morocco Square unaogharimu Sh. bilioni 137.5 ulisimama tangu mwaka 2017 kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo ya kifedha na mabadiliko ya baadhi ya maboresho kwenye maeneo ya majengo hayo.

Alisema, kwa sasa ujenzi huo unaojumuisha nyumba za makazi kwa ajili ya kuuza na kupangisha, maduka makubwa ya biashara (Mall), ofisi, kumbi za sinema, benki pamoja na hoteli unaendelea chini ya Kampuni ya Estim Construction na umefikia asilimia 90.

Dk. Mabula alisema, haileti maana mradi huo kutokamilika mapema wakati serikali ilishaliruhusu NHC kukopa fedha kwa ajili ya kukamilisha.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi huo wa Morocco Square pamoja na wa Mji wa Kawe, mkoani Dar es Salaam.

"Mradi huu wa Morocco Square umesimama kwa takriban miaka mitatu sasa, pamoja na changamoto zilizopo ninawataka mharakishe ujenzi wake ili kufikia mwisho wa mwaka huu wa fedha 2022/ 2022, mradi huu uwe umekamilika na kuanza kutumika ili shirika liweze kupata mapato.

Msimamo wa serikali ilikuwa ni kuona ile miradi iliyosimama inakamilishwa haraka na vipaumbele vilikuwa mradi wa Morocco Square na ule wa Dodoma," alisema Dk. Mabula.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani, alimwahidi Dk. Mabula kuwa Shirika hilo kwa kushirikiana na Mkandarasi watajitahidi kuhakikisha ujenzi wa mradi huo unakamilika katika muda alioagiza na kuzishughulikia baadhi ya changamoto ndani ya kipindi cha wiki moja.

" Naibu Waziri naomba nikuhakikishie kuwa, tutafanya kila jitihada kwa kushirikiana na mkandarasi kukamilisha mradi huu kama ulivyoagiza na hizi baadhi ya changamoto naomba utupe wiki moja tutakuwa tumezishughulikia," alisema Dk. Banyani.

Akizungumzia mradi wa Mji wa Kawe, Dk. Mabula alilitaka Shirika hilo kuharakisha mazungumzo ya uwekezaji na Mwekezaji Mwenza Kampuni ya Al-Gurey-Dubai, kuhusiana na mradi huo na kusisitiza kuwa, ni vizuri NHC ikawa mipango thabiti ya uendelezaji mji huo.

"Kuhusu mradi wa Kawe ni vizuri kujua future plan ya eneo na ni vizuri kila eneo la Shirika la Nyumba likafanyiwa maandalizi ya kitu kinachotaka kufanyika. Yale maeneo ambayo ni 'prime' myaainishe na kuyaendeleza maana hata NHC inaweza kunyang'anywa," alisema Dk. Mabula.



Meneja Mkuu wa Uhusiano wa Kiwanda cha Sukari cha Kilombero, Joseph Rugaimukamu (wapili kulia), akitoa maelezo kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela (kushoto), kuhusu maandalizi ya ujenzi wa kiwanda kipya cha sukari wakati alipotembelea hivi karibuni kiwandani hapo, (wapili kushoto) ni Mkurugenzi Mtendaji wa kiwanda hicho, Guy Williams na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godigod. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yakusudia kujenga majosho 178

**Na Mbaraka Kambona,** BUNDA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema katika mwaka huu wa fedha 2021/2022 serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imepanga kujenga majosho ya kuogeshea ng'ombe 178, ili kuiepusha mifugo na magonjwa yanayosababishwa na kupe na maradhi mengine yanayoambatana na kutokuogesha mifugo hiyo.

Waziri Ndaki aliyasema hayo katika ziara yake ya kukagua miundombinu ya majosho iliyopo katika Wilaya ya Bunda, mkoani Mara, juzi. Akiongea na wafugaji wanaofanya shughuli zao katika vijiji vya Salamakati na Kisarakwa katika wilaya hiyo, alisema kuwa lengo la serikali ni kuweka josho kwenye kila kijiji kilicho na ng'ombe. "Josho ni zahanati ya mifugo, hivyo sisi Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunataka tuweke kila mahali ili wafugaji waweze kuogesha mifugo yao kuepukana na kupe na magonjwa mengine yanayotokana na kutokuogesha mifugo," alisema.

Aliongeza kuwa mipango iliyopo ni kuendelea kuifanya mifugo iwe na afya njema jambo ambalo litasaidia kuongeza tija katika ufugaji ikiwamo kuuza mifugo hiyo kwa bei nzuri.

Aliwataka wafugaji hao na wananchi kwa ujumla kuendelea kutunza miundombinu ya majosho iliyopo katika maeneo yao na ile itakayojengwa kwa sababu kwa kufanya hivyo kutasaidia uogeshaji wa mifugo kuwa endelevu. Naye Mbunge wa Bunda, Boniphace Getere, alimwomba Waziri Ndaki kuhamishia hela za ujenzi wa majosho katika halmashauri ili iwe rahisi kuzifuatilia tofauti na ilivyo sasa hela za ujenzi zinatoka wizarani jambo ambalo linaleta ugumu katika ufuatiliaji na kusababisha miradi ya ujenzi wa majosho kuchelewa kumalizika.

## Tanzania, Misri zatatua vikwazo vya kodi

**Na Benny Mwaipaja,** CAIRO- MISRI

TANZANIA na Misri zimekubaliana kuondoa changamoto ya utozaji wa kodi mara mbili kwenye bidhaa zinazoingia au kutoka katika nchi hizo.

Lengo la makubaliano hayo ni kusisimua biashara na kukuza mauzo nje ya nchi yatakayoongeza upatikanaji wa fedha za kigeni.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema hayo baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Waziri wa Fedha wa Misri, Dk. Mohamed Maait, mjini Cairo nchini Misri.

Mawaziri hao wa Fedha wa Tanzania na Misri wameafikiana kushirikiana katika nyanja mbalimbali za kukuza uchumi wa nchi hizo mbili ikiwamo kutangaza fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini.

"Tumekubaliana kuendeleza ushirikiano katika eneo la kujengeana uwezo katika masuala ya kikodi lakini pia tutasaini makubaliano ya kuondoa utozaji wa kodi mara mbili kwenye bidhaa zinazotoka kwenye nchi zetu," alisema Dk. Nchemba.

Alisema Tanzania na Misri zina uhusiano wa kimkakati na hivi sasa mkandarasi anayejenga mradi mkubwa wa uzalishaji umeme wa Bwawa la Nyerere anatoka Misri, na kwamba katika eneo hilo wamekubaliana namna ya kufanikisha mradi huo ikiwamo kutafuta fedha za kuukamilisha.

Dk. Nchemba alisema kuwa wamekubaliana pia kutafuta wawekezaji watakaoleta teknolojia na mitaji nchini kwa kuwekeza kwenye maeneo yatakayotumika kuzalisha ikiwamo sekta ya kilimo.

"Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan aliwapokea wawekezaji kutoka nchini Misri, tunaweza kutumia fursa za uhaba wa ardhi kwenye nchi yao kuwavuta kuja kuwekeza kwenye shughuli za kilimo kupitia vyanzo vya fedha za kigeni kutoka kwenye kampuni zao," aliongeza Dk. Nchemba.

Aliongeza kuwa wamejadili na kuangalia namna ya kutumia nishati ya gesi inayozalishwa nchini Tanzania kuzalisha umeme kutokana na uzoefu wa nchi hiyo katika eneo hilo la matumizi ya gesi hatua iliyoifanya kuzalisha nishati ya umeme kwa wingi na ziada kuuza nchi za nje.

"Wana maslahi katika jambo hilo kwa sababu litapunguza pia uharibifu wa mazingira na kusaidia maji mengi kwenda Ziwa Victoria, maji ambayo yanatumiwa na nchi yao kwa hiyo kuna mambo mengi yanayotuunganisha, alisisitiza Waziri Nchemba.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango-Zanzibar, Jamal Kassim Al, alisema kuwa suala la kuhimiza uwekezaji kutoka Misri lilipewa kipaumbele na kutaja fursa ambazo nchi itanufaika kutokana na uwekezaji huo.

"Misri ni moja ya nchi zilizoendelea sana katika masuala ya ujenzi wa miundombinu kwahiyo tumeona tuna fursa kubwa ya kufanyakazi na kampuni kubwa za Misri kwa kujenga na kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo," alisema Ali.

Alisema walimweleza Waziri wa Fedha wa Misri, Dk. Mohamed Maait, kuhusu fursa mbalimbali za uweezaji zilizoko Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, na kwamba wanatarajia masuala ya uwekezaji na biashara yatafunguka zaidi kwa manufaa ya pande zote mbili.

# Waomba serikali kuharakisha mabadiliko Sheria ya Ndoa

**Na Zuwena Shame**

WADAU wa masuala ya haki za mtoto wa kike nchini wameiomba serikali kuharakisha utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ambayo baadhi ya vifungu vina upungufu.

Mahakama Kuu nchini mwaka jana ilisimamia hukumu ya awali ya vifungu vya Sheria ya Ndoa ya nchini vinavyopingana na Katiba kwa kuweka umri tofauti wa kuoa au kuolewa kati ya mtoto wa kike na wa kiume.

Wadau hao walitoa ombi hilo jijini Dar es Salaam jana wakati wa mjadala uliofanyika kwa njia ya mtandao uliolenga kujadili jinsi gani janga la corona nchini lilivyochangia wimbi la ndoa za utotoni na nini cha kufanya ili kupunguza.

Mmoja wa wadau hao, Mkuu wa Programu kutoka Taasisi ya Tanzania Gender Networking Program (TGNP), Joyce Mkina, alisema kuwa mchakato wa mabadiliko ya Sheria ya Ndoa hasa kipengele cha umri sahihi wa mtoto wa kike kufunga ndoa, inaweza kuchangia ndoa za utotoni kuendelea iwapo mchakato huo utachelewa.

Mkina alisema kuwa tangu Mahakama Kuu ikubali maombi hayo utekelezwaji wa mchakato wa sheria hiyo bado unasuasua.

Alisema sheria hiyo itakapobadilishwa na kuanza kutekelezwa nchini kwa watakaobainika kukiuka kuchukuliwa adhabu kali, ndoa za utotoni zitapungua kama sio kuisha kabisa.

"Katika kipindi cha janga hili la corona ndoa za utotoni zimeongezeka mara dufu hasa vijijini na hii yote ni kutokana na sheria kukinzana. Kwani bado inahalalisha umri wa mtoto wa kike ni miaka 15 ambapo wengi wao ni wanafunzi," alisema Mkina.

Aidha, alisema kuwa corona pia imesababisha watoto wa kike kufanyiwa vitendo vya ukatili ndani ya kaya zao kutokana na hali ya kiuchumi kuwa ngumu na wazazi kushindwa kuzuia sonona kutokana na shughuli nyingi za kiuchumi kusimama.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Hope for Girls and Women in Tanzania, Robhi Samwelly, alisema hali duni ya kiuchumi imekuwa changamoto kubwa katika suala la ndoa za utotoni hivyo ni muda sahihi kumwezesha mwanamke kiuchumi.

Naye Mwanasheria Rachel Magege, kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), alisema Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 bado inaipa uhalali umri wa miaka 15 kuwa sahihi kwa mtoto wa kike kuolewa.

"Mimi binafsi niko mstari wa mbele katika kupigania sheria hii iweze kubadilishwa na hatimaye mtoto wa kike anapata elimu stahiki bila vikwazo. Naomba tushirikiane kwa pamoja kuweza kusukuma mijadala muhimu itakayopelekea sheria hii kubadilishwa," alisema.

Aliongeza kuwa ni vyema pia elimu zaidi itolewe kwa wazazi wenyewe hasa vijijini ya umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike itawafanya waondokane na umaskini.




Mshindi wa mbio za Familia Marathon 2021, Aisha Ibrahim (katikati), akipokea cheti kwa Mkuu wa Mauzo na Uendeshaji wa Kampuni ya KP Motorz, Lucas Jackson, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mwenyekiti wa Familia Marathon, Francisca Alphonce. KP Motorz ilitoa zawadi ya gari aina ya Toyota Passo kwa mshindi huyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yalipongeza Jukwaa la Misitu Afrika

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imesema inatambua kazi kubwa inayofanywa na Jukwaa la Misitu Afrika (AFF), kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuelimisha jamii kuhusu nafasi ya misitu kwenye mabadiliko ya tabianchi, namna ya kukabili na kupunguza hali hiyo huku maisha ya watu na viumbe yakiendelea.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, wakati akifungua mafunzo ya misitu kwa wataalamu wa sekta hiyo kutoka nchi za Tanzania, Burkna Faso, Nigeria, Kenya, Malawi, Ethiopia, Msumbiji, Cameroon, Zambia na Zimbabwe.

Katika hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Mkuu wa Chuo cha Misitu, Wanyamapori na Utalii cha Chuo Kikuu cha Kilimo SUA, Prof. Suzana Augustino, alisema mchango wa msitu kwenye mabadiliko ya tabianchi ni mkubwa na unapaswa kutambuliwa kwa kuwa una msaada mkubwa.

Aliwapongeza AFF kwa mchango muhimu kwenye maendeleo ya misitu barani Afrika kupitia mfumo wake wa usimamizi wa sera ya sayansi, ambao umekuwa na manufaa kwa maendeleo na mchakato wa maamuzi kuhusu misitu kwenye nchi mbalimbali.

Alisema kuna fursa nyingi zilizoletwa na mabadiliko ya tabia nchi kwenye sekta ya misitu ambayo inahitaji kujenga uwezo wa kuelezea na kuziunganisha na utekelezaji wa mipango ya kimataifa, Agenda ya Umoja wa Afrika 2023 na mipango ya maendeleo ya nchi.

"Utayari wa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), sekta binafsi na jamii unahitaji uelewa wa kutosha kwenye hatua zinazochukuliwa, AFF imekuwa mstari wa mbele kuwajengea uwezo wanachama wa mtandao ambao ni wataalamu wa misitu wenye mawazo chanya na ya kina kuhusu misitu na mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Awali, Katibu Mtendaji wa AFF, Prof. Godwin Kowero, alisema jukwaa hilo lilianzishwa mwaka 2006/07 na liliona changamoto zilizopo zitatatulika lakini mazingira yamebadilika na sasa kuna ongezeko la joto na changamoto zake ambavyo vinaumiza vichwa vya wataalamu duniani.

Kwa mujibu wa Prof. Kowero, kukosekana kwa majisafi na salama ni tatizo kubwa kwa sasa linalotishia uhai wa binadamu, wanyama na viumbe wengine wanaoishi ardhini na linahitaji nguvu ya pamoja kupunguza athari.

"Mara kadhaa tunasikia watu wamekufa kwa kiu ya maji lakini ongezeko la migogoro baina ya wanyama na binadamu wengi ni wakulima wadogo ambao wana nafasi kubwa na hapa ndiyo tunaona misitu na miti kama suluhisho la matatizo haya," alisema.

Naye Prof. Suzana ambaye ni Mjumbe wa Baraza la AFF, alisema ni lazima nchi ziipe kipaumbele agenda ya msitu kwa kuwa siyo kawaida mvua kuchelewa kama sasa na kwamba athari ni kubwa kwa wanyama na biandamu.

"Ukienda kwa wakulima hali ni mbaya mazao hayajaota na yaliyoota yamekauka, mifugo inakufa na bei imeshuka kiasi kwamba hawaoni faida huku mingine ikifa, misitu ni muhimu sana katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

# Wafugaji sasa waongezewa faini mifugo kuingia hifadhini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, ametangaza rasmi kwa wafugaji watakaothubutu kuingiza mifugo katika Hifadhi ya Jamii ya Wanyamapori ya Iluma watatozwa faini ya Sh.100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe badala ya Sh. 50,000.

Uamuzi huo umetolewa baada ya malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafugaji wakidai kuwa mifugo yao inapoingia Iluma ambako faini ni Sh. 50,000 inatolewa na askari wa TANAPA na kisha huingizwa katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere ambako tozo yake ni Sh. 100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Ulanga, mkoani Morogoro, Dk. Ndumbaro, alisema amefikia uamuzi huo ili kuwapa nafasi wafugaji wataokamatwa wakiwa wameingiza mifugo yao kati ya hifadhi hizo kuamua kulipa kiasi hicho cha fedha kwa uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere au kwa uongozi wa Iluma kwa vile kote faini ni sawa.

Kwa mujibu wa taarifa, Iluma ni hifadhi ya wanyamapori inayomilikiwa jamii ambayo ni muunganiko wa vijiji 14 ambavyo vilitoa ardhi kwa ajili ya shughuli ya uhifadhi na pia ni hifadhi ambayo inapakana na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

" Habari ya kwamba ng'ombe wangu waliingizwa katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere itakuwa haipo kwa sasa kwa sababu faini ni sawa na ya Hifadhi ya Iluma," alisisitiza Dk. Ndumbaro.

Alisema kumezuka tabia ya wafugaji kujichagulia kiasi cha faini ya kulipa mifugo yao inapokamatwa ndani ya hifadhi hiyo na kusisitiza kuwa jambo hilo kamwe halikubaliki.

Alisema mfugaji atakayekuwa na hatia hana haki ya kuchagua adhabu, huku akisisitiza kuwa hali hiyo imesababisha wafugaji kusema uongo kuwa ng'ombe wao wanapokamatwa katika Hifadhi ya Iluma waswagwa katika Hifadhi ya Nyerere ambako faini yake ni kubwa, jambo ambalo sio kweli.

"Kwa mamlaka niliyonayo kama Waziri mwenye dhamana, natangaza kuanzia leo faini ni kiasi cha Sh.100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe," alisisitiza Dk. Ndumbaro.

Akifafanua uamuzi huo wa kutoza Sh.100,000 kwa kila kichwa cha ng'ombe atakayekutwa ndani ya Hifadhi ya Iluma, Dk. Ndumbaro alisema anaitumia faini hiyo kutoka katika kifungu cha sheria kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) pamoja na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

# Mashirika yaingia kukabili ukatili kwa watoto

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MASHIRIKA mawili yasiyo ya kiserikali, ambayo yanatetea haki za watoto yameunganisha nguvu za pamoja katika kufanya kampeni ya kutokomeza matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto, likiwamo na tatizo la mimba na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga.

Mashirika hayo ni Agape lililoko mkoani Shinyanga, pamoja na Shirika la Global Network of Religion For Children (GNRC) Tanzania lenye makao yake makuu jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa GNRC, Joyce Mdachi, alibainisha hayo juzi kwenye warsha na viongozi wa dini, wazazi, dawati la jinsia, viongozi wa kata, maofisa maendeleo na ustawi wa jamii Manispaa ya Shinyanga, iliyokuwa na lengo la kujadili na kupanga mpango kazi wa kutokomeza matukio ya ukatili dhidi ya watoto.

Alisema baada ya kusikia kazi za Shirika la Agape ambazo inazifanya za kupigania haki za watoto mkoani Shinyanga, likiwamo suala la mimba na ndoa za utotoni, waliona ni vyema waje Shinyanga kuunganisha nguvu za pamoja na Shirika hilo, ili kutokomeza matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto.

"Baada ya kuunganisha nguvu na Shirika hili la Agape, tukaona ni vyema tukutane na watu ambao wanashirikiana nao katika mapambano haya ya kupinga ukatili dhidi ya watoto wadogo, ili tupange mpango mkakati wa kuendeleza mapambano haya, na watoto wetu waishi salama na kutimiza ndoto zao,"alisema Mdachi.

"Matarajio yetu Shirika la GNRC baada ya kuunganisha nguvu na Shirika la Agape na nyie wadau mkiwamo viongozi wa dini, ni kubadilisha mitazamo na tamaduni ambazo zinaleta madhara kwa watoto, mabadiliko ya sera na sheria ili kumlinda mtoto wa kike, pamoja na jamii kuwa na vitega uchumi mbadala na siyo kutegemea kuozesha mtoto," aliongeza.

Naye Mkurugenzi wa Agape, John Myola, alisema matukio ya ukatili mkoani humo bado yapo ambapo wadau, mashirika, jamii na viongozi wa dini wanapaswa kuunganisha nguvu ya pamoja kupaza sautijuu ya kutokomeza vitendo vya kingono dhidi ya watoto.

Sheikh Hamisi Nkingo kutoka Msikiti wa Mabambase Ngokolo Manispaa ya Shinyanga, alisema jamii inapaswa kubadilika na kuacha kuwafanyia ukatili watoto wa kike, na kwamba matukio hayo asilimia kubwa hufanywa na watu wa karibu.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, akimtunuku shahada ya uzamili mmoja wa wahitimu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) katika mahafali ya 37 yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri afagilia kozi usafiri wa maji, reli

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imekipongeza Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kwa kuanza kutoa mafunzo ya usafiri wa njia ya maji pamoja na kuongeza wigo wa utoaji mafunzo ya reli.

Akizungumza katika mahafali ya 37 ya chuo hicho jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alisema kozi hizo ni muhimu sana kwa Taifa kwani zitapunguza mzigo kwa serikali wa kugharamia mafunzo haya nje ya nchi ambayo hutolewa kwa gharama kubwa.

"Nimefarijika kusikia kwamba chuo kimeendelea kutanua wigo wa kutoa mafunzo katika sekta hii muhimu ya uchukuzi, ikiwa ni pamoja na kujiimarisha katika njia zote za usafirishaji yaani usafiri wa anga, majini, reli, barabara na usafiri kwa njia ya mabomba. Nawapongeza sana," alisema.

Waitara aliongezea kuwa serikali inafahamu vizuri changamoto zinazokikabili chuo ikikiwamo uchakavu wa miundombinu na majengo, uhaba wa ofisi za wahadhiri na uhaba wa nafasi za mabweni kwa wanafunzi.

"Serikali itaendelea kushirikiana na chuo katika kuhakikisha changamoto hizi zinapatiwa ufumbuzi. Aidha, ninauagiza uongozi kuendelea kutumia mapato ya ndani katika kuendeleza na kuboresha miundombinu ya chuo," alisema.

Alisema kuwa serikali imenunua ndege mbili kwa ajili ya mafunzo ya urubani, injini mbili kwa ajili ya mafunzo ya uhandisi wa ndege na mock ups kwa ajili ya mafunzo ya wahudumu wa ndani ya ndege kwa NIT.

Aidha, alisema kuwa serikali imetoa ardhi katika eneo la KIA lenye ukubwa wa hekta 60, ambalo litakuwa maalum kwa mafunzo ya taaluma za usafiri wa anga.

"Serikali inafanya haya yote ili kukiwezesha chuo kitoe elimu bora na kuandaa wataalamu wa kutosha wa Sekta ya Uchukuzi na Usafirishaji. Hivyo, nitoe wito kwa chuo, vifaa hivi ambavyo serikali imenunua kwa gharama kubwa vitunzwe ili Watanzania wengi wanufaike katika kupata mafunzo," alisema.

Naye Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa, alisema kuwa idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka hivyo kupelekea ongezeko la wataalam katika sekta ya uchukuzi.

"Katika kipindi cha miaka mitano idadi ya wanafunzi imeongezeka kwa asilimia 67 kutoka 7,752 mwaka 2016/2017 hadi wanafunzi 12,980 mwaka 2021/2022," alisema.

Prof. Mganilwa alisema kwa sasa NIT ina jumla ya wafanyakazi 346 ikiwa wanataaluma ni 224 na waendeshaji wapatao 122, ingawa hii ni ndogo hasa kwa wanataaluma ikilinganishwa na mahitaji halisi ya chuo.

"Hivyo, chuo kinalazimika kutumia fedha nyingi kuwalipa wahadhiri wa muda ili kuziba upungufu uliopo. Tunaamini katika mwaka huu wa fedha tutaweza kupata kibali cha ajira mpya," slisema.

Aliongeza: "Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo wahadhiri na watumishi wake kwa kuwapeleka masomoni ndani nan je ya nchi ili kuongeza kiwango cha maarifa na ujuzi wao ambapo katika mwaka wa masomo 2020/21 jumla ya watumishi 65 walikuwa masomoni kati yao watumishi 30 wanasoma katika ngazi ya shahada ya uzamivu (PhD), 30 wanasoma shahada ya uzamili na watano wanasoma shahada ya kwanza na astashahada."

Prof Mganilwa alisema kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania (TAA) imekipatia Chuo eneo lenye ukubwa wa hekta sitini (60) lililopo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kuendeshea mafunzo ya usafiri wa anga ikiwemo kozi ya urubani pamoja na uhandisi wa matengenezo ya ndege.

# Vitendo vya wanaume kutelekezea wake watoto vyapungua

**Na Happy Severine,** ITILIMA

VITENDO vya wanawake kutelekezewa watoto na waume zao vimeendelea kupungua wilayani Itilima mkoani Simiyu kutoka matukio 200 mwaka 2018 hadi 102 kwa mwaka wa fedha 2020/ 2021.

Matukio hayo yameelezwa kupungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kasi ya utolewaji wa elimu ya kupinga vitendo vya ukatili inayotolewa na serikali, ofisi ya maendeleo ya jamii wilayani humo na wadau mbalimbali kupitia vyombo vya habari.

Akisoma taarifa ya hali halisi ya matukio ya ukatili kwa wanawake na watoto jana kwenye kilele cha Siku 16 za Kupinga Ukatili yaliyofanyika katika Kata ya Chinamil, Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Itilima, Felicia Mbwambo, alisema elimu imesaidia vitendo vya ukatili kuendelea kupungua siku hadi siku sambamba na jamii kushiriki moja kwa moja kutoa taarifa na ushahidi wa matukio hayo.

"Matukio au kesi za wanawake kutelekezewa watoto au kutopatiwa matunzo na waume zao yameanza kupungua na kadri elimu inavyotolewa vitendo hivyo vitakomeshwa kabisa," alisema.

Mbwambo alifafanua kuwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kati ya matukio 102 ya wanawake kutelekezewa watoto, matukio 28 yalifikishwa mahakamani na 74 yalipatiwa suluhu kwenye kitengo cha ustawi wa jamii na kuiomba jamii ishiriki moja kwa moja kutoa taarifa na ushahidi sehemu husika ili vitendo hivyo viweze kutokomea.

Aidha, Mbwambo alisema vitendo vya wanaume kuwatelekezea wanawake watoto vimesababisha watoto wengi kukosa matunzo na mahitaji yao ya msingi kama inavyotakiwa.

Nae Meneja Shirika lisilo la Kiserikali la World Kanda ya Nzega, Jackline Kaihura, aliwataka wanawake kutoruhusu vitendo hivyo vifanyike dhidi yao, huku akiwasihi watoto wasikubali kunyanyaswa wakati haki zao za msingi wanazijua.

Aliongeza kuwa endapo watatendewa vitendo ambavyo vyenye viashiria vya ukatili ndani yake watoe kutoa kwa walimu wao.

"Msikubali kunyamaza mnapotendewa vitendo vya ukatili...kama nyumbani mnaogopa kuwaambia wazazi basi waambieni walimu wenu ili wawasaidie," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Itilima, Faiza Salim, aliwasihi wanaume kuchapa kazi ili kutunza familia na si kuwachapa wala kuwatelekeza wake zao kwa kukwepa majukumu.

Aidha, alilitaka Jeshi la Polisi wanapopelekewa kesi za matukio ya ukatili kwa kijinsia na wanawake wayafanyie kazi mapema badala ya mashauri hayo kukaa muda mrefu.

## HCCGWT yataja mwarobaini wa mimba za utotoni

**Na Elizabeth Zaya**

OFISA Maendeleo wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, Marietha Mkozi, amesema elimu ya ujasiriamali kwa vijana na wanawake ni muhimu kwa sababu itasaidia kupunguza umaskini na kuwaondoa katika hatari ya kuingia kwenye vishawishi vya mahusiano ya kimapenzi yasiyo salama na mimba za utotoni.

Aliyasema hayo mkoani Katavi katika semina ya kuwajengea uwezo vijana na wanawake namna ya kuendesha biashara ndogo kwa kuomba mikopo kwenye taasisi za fedha na taasisi za umma, usafi wa mzingira, afya ya uzazi na ujinsia pamoja na namna ya kujikinga na ugonjwa wa COVID-9 iliyodhaminiwa na Taasisi ya inayojishughulisha na kuwajengea uelewa vijana juu ya uzazi salama (HCCGWT).

Alisema vijana wanapojishughulisha na kazi mbalimbali ikiwamo kuingia kwenye biashara hususani wa kike, wanakuwa na uwezekano mkubwa wa kukwepa vishawishi ambavyo vimekuwa vikiwasabaishia baadhi yao kuambukizwa maradhi ikiwamo virusi vya Ukimwi.

Pia, alisema wanapojiunga katika vikundi mbalimbali vya biashara vinawasaidia kujifunza mambo mengi ya kibiashara na namna ya kutafuta masoko na kuboresha zaidi biashara zao.

"Na kwenye mafunzo kama haya, tunawafundisha vijana hawa namna ya kuwa na malengo na kuendesha biashara ambazo ni mahitaji ya kila siku kwenye jamii, kuhakikisha wanakuwa wabunifu, kubuni mawazo mapya kila siku na kutoa huduma bora na kuziongezea thamani bidhaa zao," alisema Mkozi.

"Tunawaelimisha kwamba wazo lolote la biashara halitaleta matunda chanya endapo halitafanywa kwa ubunifu na umakini zaidi." Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa HCCGWT, Halima Lila, alisema jumla ya vijana na wanaake 40 walipewa mafunzo hayo kutoka katika mkoa huo wa Katavi. Alisema kupitia mafunzo hayo, vijana wengi walisema wako tayari kuwa mabalozi wa kutoa elimu kwa wenzao kuhusu namna ya kuanzisha biashara ndogo wakiamini ndilo suluhisho la kupunguza mimba za utotoni zinazosababishwa na vijana wengi kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi mapema.

"Na kupitia mafunzo haya, tayari baadhi yao wameanza kujiunga katika vikundi vya ujasiriamali kwa ajili ya kuanzisha biashara zao na tunaamini kupitia vikundi hivyo watapata uzoefu, watakuwa wazalishaji wakubwa na wataondokana na umaskini," alisema Lila.

# Mhagama ataka mifumo ya kulinda afya viwandani

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ametoa wito kwa wenye viwanda kuimarisha mifumo ya kulinda afya na usalama wa wafanyakazi.

Mhagama amesema kuwa lengo ni kuleta tija katika uzalishaji na ukuaji wa biashara zao.

Alitoa wito huo alipofanya ziara katika kiwanda cha Alaf Limited kinachozalisha mabati na bidhaa nyinginezo za chuma pamoja na Kiwanda cha Kioo Limited kinachozalisha bidhaa mbalimbali za vioo, viwanda hivyo vipo Manispaa ya Temeke katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Katika maelezo yake ya awali kwa menejimenti za viwanda husika, Waziri Mhagama alieleza kwamba dhumuni la ziara yake ilikuwa ni kuangalia jinsi viwanda hivyo vinavyozingatia masuala ya usalama na afya kwa wafanyakazi pamoja na masuala mengine yanayohusu kazi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanzania.

"Kama walivyoeleza katika taarifa yao, kiwanda hiki kina miaka 61 tangu kilipoanzishwa na serikali yetu ni mbia wa kiwanda hiki hivyo tunapoadhimisha miaka 60 ya Uhuru tumeona ni vema tukatembelea kiwanda hiki ili tuweze kuona katika kipindi hicho chote kiwanda kimepata mafanikio gani?" Alisema Mhagama na kuongeza; "Kupitia taarifa iliyowasilishwa na viongozi pamoja na yale niliyoyaona nilipotembelea maeneo tofauti katika viwanda hivi nimefarijika kuona wamefanikiwa katika mambo mengi ikiwamo kuimarisha mifumo ya usalama na afya kwa wafanyakazi, maslahi ya wafanyakazi yameendelea kuboreshwa kupitia uwapo wa mikataba ya hali bora.

Aidha, nimeona kiwango cha kodi mnachochangia kwenye mapato na mfuko mkuu wa serikali ni kikubwa ambapo kwa upande wa Alaf Limited kwa miaka mitano iliyopita kiwanda kimechangia zaidi ya Sh. bilioni 290 kiwango ambacho kinaridhisha."

Katika ziara hiyo, viongozi wa viwanda vyote viwili waliwasilisha taarifa fupi kuhusu utendaji wao, mafanikio pamoja na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo katika uzalishaji, miongoni mwa mafanikio yaliyoelezwa ni pamoja na kutoa ajira za moja kwa moja zipatazo 500 kwa kila kiwanda pamoja na kuchangia kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Katika ziara hiyo Waziri Mhagama aliambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), Khadija Mwenda na watendaji wengine wa OSHA. Mwenda aliwapongeza viongozi wa viwanda vya Alaf Limited na Kioo Limited kwa kushirikiana vema na taasisi yake katika kuweka mifumo madhubuti ya kulinda nguvukazi suala ambalo ndilo jukumu la msingi la OSHA. "Kwakweli wote mliojumuika nasi katika ziara hii mmejionea jinsi viwanda hivi vilivyoweka mifumo mizuri ya kulinda afya na usalama wa wafanyakazi hivyo nawapongeza sana wenye viwanda hivi kwa kushirikiana nasi katika kutimiza wajibu wetu wa kuwalinda wafanyakazi pamoja na kulinda mitaji ya wawekezaji dhidi ya majanga mbalimbali. Aidha, nawaahidi tu kwamba tutaendelea kushirikiana nao kwani jukumu letu ni kuwawezesha wawekezaji na sio kuwakwamisha katika shughuli zao za uzalishaji," alisema Mwenda.

"Tumefarijika sana kupokea ugeni huu na tunamshukuru sana Waziri Mhagama kwa kututembelea ili kujua mafanikio na changamoto zetu na hivyo kutusaidia kuzitatua," alisema Ashish Mistry, Mkurugenzi Mkuu wa Alaf Limited.

Kwa upande wa Meneja Rasilimali Watu wa Kioo Limited, Jacob Msuya, aliishukuru OSHA kwa kuwapa miongozi ya mara kwa mara kuhusu uzingatiaji wa viwango vya usalama na afya mahali pa kazi hususan kupitia mfumo mpya wa kielektroniki wa usimamizi wa maeneo ya kazi ujulikanao kama WIMS, ambao alieleza kwamba umeondoa urasimu wa huduma za OSHA.




Meneja wa Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald, akikabidhi Tuzo ya Sayansi ya Kompyuta na Teknolojia zilizoandaliwa na Young Scientists Tanzania (YST Awards ceremony 2021) kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mzumbe Morogoro, jijini Dar es salaam kwa Innocent Mamsery (kushoto) na Sylvester Mulungu, ambao walibuni mradi wa mfumo wa kufuatilia maendeleo ya kielimu ya wanafunzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasomi wa kada ya afya HKMU waombewa mikopo

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeombwa kutoa ufadhili na mikopo kwa wanafunzi wengi wa elimu ya juu wanaosomea masuala ya afya ili kukabiliana na upungufu wa watumishi wa sekta hiyo kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), John Ulanga, wakati wa mahafali ya 19 ya chuo hicho yaliyofanyika kwenye viwanja vya chuo hicho.

Jumla ya wahitimu 309 walitunukiwa vyeti, stashahada, shahada, shahada za uzamili baada ya kufuzu taaluma zao kwa mwaka wa masomo wa 2020/2021.

Wahitimu 84 walitunukiwa Stashahada ya Uuguzi, 43 Shahada ya Uuguzi, wahitimu 171 walitunukiwa Shahada ya Udaktari wa Binadamu, 7 Shahada ya Uzamili ya Udaktari wa Binadamu katika Tiba na Afya ya Watoto, 3 Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Afya ya Jamii na mmoja Shahada ya Uzamili ya Ustawi wa Jamii.

Ulanga alisema miaka 30 ijayo idadi ya watu Tanzania itakuwa mara mbili ya idadi ya sasa hivyo kuna kila haja ya kusomesha watumishi wa kada ya afya kwa wingi sana kwani upungufu unaoonekana sasa kwa watumishi wa kada ya afya itaongezeka mara dufu miaka michache ijayo.

Alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) mwaka huu zinaonyesha kwamba daktari mmoja Tanzania anahudumia watu 20,000 badala ya idadi inayopendekezwa na shirika hilo daktari mmoja kuhudumia wagonjwa 1,000 kwa mwaka.

Hata hivyo, aliishukuru Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu HESLB kwa kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa chuo hicho na wa vyuo vingine na kwamba mikopo hiyo isingekuwapo basi idadi ya wahitimu wa chuo hicho ingekuwa ndogo.

"Nitoe rai kwa serikali kutupia jicho sekta ya elimu kwa wataalamu wa afya kwa kutoa mikopo na ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchinikwa idadi kubwa zaidi.

Nii kweli kabisa kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wanaosoma kwenye chuo chetu kwa mwaka huu walipata kiasi kidogo sana cha mkopo hasa kwenye ada," alisema Ulanga.

Nipashe
Spotika



NYOTA 10 WALIOSTAHILI KUSHINDA BALLON D'OR UK. 12

# MAKOMBE MATANO GHALI ZAIDI DUNIANI




**NYON, Uswisi**

KUSHINDA michezo na mataji ndio malengo ya msingi ya timu yoyote ya mpira wa miguu duniani. Soka limekuwa mchezo maarufu zaidi duniani na makombe yake kwenye michuano ya hadhi ya juu yanatambulika kwa mashabiki wote duniani.

Hatupaswi kuwa na hisia bora kwa timu ya soka kuliko kutwaa kombe la kipekee mwishoni mwa mashindano. Ukiwa ni mchezo unaofuatiliwa zaidi duniani, kuna fedha nyingi zimewekezwa katika 'mchezo mzuri'.

Kwa hiyo haishangazi kwamba mataji haya mahiri katika soka yanathamani kubwa katika masuala ya fedha pia.

Bila kuchelewa, hebu tuangalie mataji matano ghali zaidi katika soka la dunia hii ya leo, twende sasa...

**#5. Serie A - Euro 55,000**

Taji la Serie A, ambalo hutolewa kwa mshindi wa Ligi Kuu Italia mwishoni mwa kila msimu, hugharimu euro 55,000. Linaitwa "Coppa Campioni d'Italia" na kombe hilo limekuwa likitumika tangu msimu wa 1960-61.

Lakini hadi mwaka 2004, kombe hilo halikuwahi kukabidhiwa timu iliyoshinda kwenye uwanja. Ilikuwa kombe linapelekwa kwenye makao makuu ya klabu iliyoshinda. Utamaduni huo ulibadilika mwaka 2004 na tangu wakati huo, mshindi wa Serie A anapewa fursa ya kuzunguka nalo uwanjani.

Ingawa Ligi Kuu England, ndio ligi tajiri zaidi duniani, Kombe la Serie A ndio taji ghali zaidi kwa ligi zote Kuu za Ulaya. Hiyo inapaswa kukufanya utambue kwamba, jinsi gani Waitaliano wanathamini vitu hivi.

**#4. Kombe la Mataifa ya Afrika - Euro 127,000**

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, amepokea joto jingi hivi majuzi kwa kuyaita mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kuwa ni 'madogo'. Kocha huyo wa Ujerumani alijitetea akisema kuwa hakumaanisha kudharau mashindano hayo na kwamba nukuu yake hiyo ilipokelewa vibaya.

Ingawa alichosema Klopp kinaweza kuwa kweli, huwezi kuwalaumu Waafrika kwa kukerwa na maoni kama hayo. Baada ya yote, Kombe la Mataifa ya Afrika ni mojawapo ya mashindano ya soka bora duniani.

Thamani halisi ya Kombe la Mataifa ya Afrika ni euro 127,000 na ni ghali zaidi ya mara mbili ya Kombe la Serie A ambalo liko nyuma yake kwa thamani.

**#3. Ballon d'Or - Euro 508,000**

Pamoja na fedha hizo zote anazopata kama mshahara na kupitia mikataba ya udhamini, Lionel Messi pia ana takriban Euro milioni 3.5 katika mataji pekee ya Ballon d'Or yakiwa kwenye kabati lake. Hiyo ni kweli, zawadi ya mtu binafsi ya kifahari zaidi ya soka inagharimu zaidi ya nusu milioni ya Euro.

Tuzo ya Ballon d'Or inatolewa na Jarida la Ufaransa la France Football na anapewa heshima mchezaji aliyefanya vizuri zaidi katika ulimwengu wa soka katika kipindi cha mwaka mmoja. Messi alishinda Ballon d'Or na kuweka rekodi kwa kuibeba mara ya saba.

Taji la Ballon d'Or ni la kifahari sana na linaripotiwa kuwa na uzito wa takriban kilo 12. Ina sahani mbili za shaba zilizopambwa ili kulifanya lionekane kama mpira. Inasemekana kuwa kwa ndani limechimbwa ili kulipa umbo la duara kabla ya kuoshwa kwa dhahabu safi ili kulifanya lionekane la kifahari.

**#2. Kombe la FA - Euro Milioni moja**

Naam, hapa kuna mshangao kidogo. Kombe la Chama cha Soka cha Uingereza (FA), ambalo ndilo shindano kubwa zaidi la kombe la mtoano nchini humo, ni taji la pili kuwa ghali zaidi katika ulimwengu wa soka. Kombe hilo limekuwa na miundo miwili na kumekuwa na vikombe vitano halisi.

Kombe la sasa ni nakala ya muundo wa mwaka 2014 ambao umetengenezwa kwa kilo 6.3 za madini ya fedha. Ilimchukua saa 250, mbunifu wake, Thomas Lyte ambaye ni Muingereza kutengeneza taji hili.

Arsenal ndio timu iliyofanikiwa zaidi katika historia ya Kombe la FA. Wameshinda taji hilo mara 14. Manchester United wako nyuma katika nafasi ya pili wakiwa wameshinda mara 12.

**#1. Kombe la Dunia la FIFA - Euro Milioni 17**


Hili ndilo kombe kubwa zaidi katika soka na ni ghali zaidi kuliko yote. Kombe la Dunia la FIFA ndilo kombe la bei ghali zaidi katika kandanda ya ulimwengu. Thamani yake halisi ni euro milioni 17.

Lina vipande 18 vya dhahabu na lina uzito wa kilo 6.1. Kombe hilo ni la kifahari na muundo wake ni miili ya sura ya watu wawili wakiwa wameshikilia ulimwengu (Dunia).

Ndio kombe linalotambulika zaidi katika ulimwengu wa kandanda na tutaliona likikabidhiwa kwa timu baada ya mashindano ya Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani.

## ISIKUPITE

KIPA wa zamani wa Dynamo Moscow, Lev Yashin, ni golikipa pekee aliyeweza kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia 'Ballon d'Or', ambapo alifanya hivyo mwaka 1963.



NIPASHE JUMATATU DESEMBA 13, 2021



Extra Time

# NYOTA 10 WALIOSTAHILI KUSHINDA BALLON D'OR

**LONDON, England**

TUZO ya Ballon d'Or imekuwa ikitawaliwa na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo kwa karne hii. Wachezaji wote wawili wameshinda tuzo hiyo mara 12 kati yao. Luka Modric pekee (2018) ndiye aliyewashinda wawili hao.

Hata hivyo, kumekuwa na matukio ambapo ilionekana kuwa mshindi wa Ballon d'Or hakustahili.

Messi ameshinda tuzo ya Ballon d'Or mara saba. Si rahisi kufikia mafanikio kama hayo. Licha ya ushindi wake, wakati mwingine ilionekana kuwa washindani wake hawakustahili kupoteza pia.

Wachezaji kumi katika historia ya Ballon d'Or wameshinda tuzo hiyo zaidi ya mara moja. Hilo humfanya mtu kujiuliza orodha ya washindi itakuwaje ikiwa mchezaji anastahili kushinda mara moja tu.

Kwa maelezo hayo, hapa tunawaangalia wachezaji 10 ambao wangeweza kushinda tuzo ya Ballon d'Or katika kipindi cha miaka kumi iliyopita:

**#10. Robert Lewandowski (Bayern Munich - 2021)**

Kwa sababu ya janga la COVID-19, Ballon d'Or haikutunukiwa mchezaji yeyote mwaka jana 2020. Mwaka huo, Robert Lewandowski alifanya kazi ya ajabu akiwa na Bayern Munich na Poland.

Alifunga mabao 41 kwenye Bundesliga msimu wa 2020-21, na hadi sasa msimu huu, amefunga mabao 16. Mshambuliaji huyo wa Poland ni tishio kubwa mbele ya lango. Amekuwa mmoja wa washambuliaji bora katika mchezo huo kwa miaka michache iliyopita.

Licha ya kuwa na wakati mzuri mnamo mwaka 2021, Lewandowski alimaliza nafasi ya pili kwenye Ballon d'Or ya 2021, akipoteza dhidi ya Messi kwa alama 33. Kwa kuzingatia uchezaji wake katika misimu michache iliyopita, mshambuliaji huyo wa Bayern Munich alistahili tuzo ya Ballon d'Or, haswa katika miaka miwili iliyopita.

**#9. Virgil Van Dijk (Liverpool - 2019)**

Moja ya sababu kuu nyuma ya mafanikio ya Liverpool ni uwapo wa Virgil van Dijk. Beki huyo wa Uholanzi alikuwa kwenye rada za 'Wekundu' hao kwa muda mrefu kabla ya kusajiliwa mwaka 2018.

Beki huyo wa kati wa zamani wa Southampton ni mkali, mwenye busara na mwerevu katika safu yake ya ulinzi. Uwezo wake wa angani pamoja na ukali wake unamfanya kuwa beki hodari sana. Kiwango chake katika msimu wa 2018-19, kilisaidia Liverpool kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuwa washindi wa pili katika msimu uliopita.

Hata kwenye Ligi Kuu England, Mholanzi huyo alionekana imara sana akiisaidia Liverpool kushinda taji hilo msimu wa 2019-20. Virgil van Dijk alitajwa kushinda Ballon d'Or 2019, lakini akapitwa na Messi kwa pointi saba pekee.

Kama si kwa Messi, beki huyo mwenye umri wa miaka 30, angeshinda tuzo hiyo kwa raha mwaka huo. Hiyo ni kwa sababu mchezaji aliyefuata alikuwa amepitwa zaidi ya pointi 200 nyuma ya Van Dijk.

**#8. Luka Modric (Real Madrid - 2018)**

Luka Modric amekuwa mchezaji wa ajabu wa Real Madrid. Kwa mbinu yake ya ushupavu na ya kutochoka uwanjani, kiungo huyo wa kati wa Croatia amekuwa na mchango mkubwa kwa 'Los Blancos' hao.

Mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur, ameshinda tuzo nyingi akiwa na Real Madrid. Baada ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2017-18, aliipeleka Croatia kwenye fainali za Kombe la Dunia mwaka 2018.

Croatia waliishia kuwa washindi wa pili wakati Ufaransa ikibeba taji, lakini Modric alikuwa amefanya vya kutosha kushinda Ballon d'Or. Ndiye mchezaji wa kwanza kuwashinda Ronaldo na Messi tangu Mbrazil Kaka mwaka 2007.

**#7. Gianluigi Buffon (Juventus - 2017)**

Ballon d'Or ni nadra kuona makipa wakishinda tuzo hiyo. Kwa kweli, Lev Yashin anabaki kuwa golikipa pekee aliyeshinda tuzo hiyo. Alifanya hivyo mwaka 1963 alipokuwa akiichezea Dynamo Moscow.

Tuzo ya Ballon d'Or 2017 ilimshuhudia Ronaldo akishinda kwa mara ya tano. Hakukuwa na shaka juu ya sifa zake mwaka huo, kutokana na uchezaji wake mzuri pale Real Madrid na Messi alimaliza nafasi ya pili kwa tofauti ya zaidi ya pointi 250.

Gianluigi Buffon pia aliifanyia Juventus vema mwaka huo, akiwasaidia kushinda Serie A na kuishia kama washindi wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hatimaye alimaliza wa nne katika tuzo ya Ballon d'Or 2017, nyuma ya Ronaldo na Messi.

**#6. Antoine Griezmann (Atletico Madrid - 2016)**

Antoine Griezmann alionyesha kiwango kizuri katika kipindi chake cha kwanza akiwa na Atletico Madrid. Uwezo wa mshambuliaji huyo wa Ufaransa kucheza katika nafasi tofauti ulikuja kuwafaa sana 'Rojiblancos' hao.

Alikuwa mchezaji muhimu wa Atletico na timu ya Taifa ya Ufaransa mwaka 2016. Griezmann alicheza nafasi kubwa katika michuano ya Euro 2016, ambapo Ufaransa iliishia kuwa mshindi wa pili. Atletico Madrid walifanya vema katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2015-16, ambapo walipoteza kwa Real Madrid kwenye fainali kwa mikwaju ya penalti. Griezmann alichukua nafasi kubwa katika kampeni hiyo, akifunga mabao saba. Lakini alikosa penalti yake kwenye fainali.

Tuzo ya Ballon d'Or ya 2016, ingawa, ilikuwa ya Ronaldo, kutokana na uchezaji wake mzuri Real Madrid, Griezmann alimaliza wa tatu, huku Messi akimaliza wa pili.



LEWANDOWSKI

**#5. Neymar (Barcelona - 2015)**

Neymar pengine alikuwa kwenye ubora wake alipokuwa akiichezea Barcelona. Wachezaji watatu Messi, Neymar na Luis Suarez walifanya makubwa kwenye safu ya ushambuliaji kwa 'Blaugrana' hao.

Akiwa na wachezaji hao wa kiwango cha dunia wakimzunguka, Neymar alifanya vema uwanjani. Alikuwa sehemu ya kikosi cha Barcelona kilichoshinda mataji matatu msimu wa 2015-16.

Uchezaji wake bora ulimfanya kumaliza katika nafasi ya tatu kwenye Ballon d'Or 2015, nyuma ya mshindi Messi na mshindi wa pili Ronaldo.

**#4. Manuel Neuer (Bayern Munich - 2014)**

Manuel Neuer bila shaka ni mmoja wa magolikipa bora wa kizazi chake.

Kipa huyo wa Bayern Munich alikuwa mchezaji bora wa klabu hiyo tangu alipojiunga nayo mwaka 2011. Aliwasaidia wababe hao wa Bavaria kushinda Bundesliga na DFB-Pokal msimu wa 2013-14. Jukumu la Neuer pia lilikuwa muhimu katika kusaidia Ujerumani kushinda Kombe la Dunia mwaka 2014.

Kipa huyo wa Ujerumani hatimaye alimaliza wa tatu kwenye Ballon d'Or 2014, huku Ronaldo na Messi wakimaliza mbele yake.

**#3. Franck Ribery (Bayern Munich - 2013)**

Ballon d'Or imechukuliwa na wachezaji wachache wa Ufaransa, lakini hakuna hata mmoja aliyefanya hivyo karne hii. Thierry Henry, Antoine Griezmann na Franck Ribery ndio wachezaji pekee wa Ufaransa ambao walikaribia kushinda Ballon d'Or katika karne ya 21.

Ribery alikuwa na maisha mazuri akiwa na Bayern Munich, kabla ya kuhamia Fiorentina mwaka wa 2019. Akiwa na mabao 10 na asisti 14 msimu wa 2012-13, aliwasaidia wababe hao wa Bavaria kushinda Bundesliga.

Pia alishinda DFB Pokal na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huo huo, akikamilisha mataji matatu akiwa na Bayern Munich. Hata hivyo, Ribery alimaliza wa tatu katika tuzo za Ballon d'Or 2013, akimaliza nyuma ya Messi na Ronaldo.

**#2. Radamel Falcao (Atletico Madrid - 2012)**

Radamel Falcao aliichezea Atletico Madrid kwa misimu miwili pekee, lakini alikuwa na idadi kubwa ya mabao. Mshambuliaji huyo wa Colombia alijiunga nao mwaka wa 2011 baada ya kucheza vizuri akiwa na Porto FC.

Katika misimu yake miwili akiwa na Atletico, alifunga mabao 52 katika mechi 68 za LaLiga. Hata kwenye Ligi ya Europa msimu wa 2011-12, Falcao alikuwa mzuri, akifunga mara 12 katika mechi 15.

Falcao alimaliza wa tano kwenye Ballon d'Or 2012, nyuma ya mshindi Messi. Ronaldo, Andres Iniesta na Xavi.

**#1. Xavi (Barcelona - 2011)**

Xavi bila shaka ni mmoja wa viungo bora wa kati wa kizazi chake. Kwa maono yake, pasi za kuvutia na uwezo wa ubunifu, kiungo huyo wa Hispania alikuwa mchezaji muhimu wa Barcelona.

Upatina wa Xavi na Andres Iniesta katika safu ya kiungo ilitengeneza hofu kubwa kwa safu ya ulinzi ya timu pinzani. Xavi uwezo wake sahihi wa kupiga pasi na kucheza ulimfanya kuwa tishio kubwa.

Kiungo huyo wa Hispania aliisaidia Barcelona kushinda LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2010-11. Alimaliza nafasi ya tatu kwenye Ballon d'Or ya 2011. Messi na Ronaldo wakimaliza mbele yake.

## Nukuu

"Mchezo ulikuwa mzuri na ulitawaliwa na mbinu nyingi, ndiyo maana hakukuwa na nafasi nyingi, Yanga tulicheza vizuri kipindi cha kwanza na Simba ilicheza vizuri kipindi cha pili kwa kutengeneza nafasi ambayo Diarra aliokoa. Wapinzani wetu wameimarika na tulichofanya ni kuwazuia wasipate nafasi ya kufunga," **Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi baada ya kutoka suluhu.**



"Hatupendi kuonewa, tunataka kujua kwa nini CEO wetu [Barbara Gonzalez] amezuiwa kuingia uwanjani. Hatuwezi kuvumilia mambo ya kipumbavu kama hayo, Klabu ya Simba ni kubwa, hao wanaotaka kuwapa ubingwa wakawape huo ubingwa chumbani," **Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu baada ya CEO wao kuzuiwa kuingia kwenye mechi dhidi ya Yanga juzi.**



"Nimesikitishwa sana na kitendo alichofanyiwa CEO wa Simba [Barbara Gonzalez] cha kuzuiliwa kuingia kwenye eneo la VVIP katika mchezo wa jana. Kwa nafasi ya uongozi aliyonayo CEO ni jambo la aibu kwa soka letu kukutana na kadhia kama ile. Kumvunjia heshima CEO, ni kuvunjia heshima taasisi ya Simba," **Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed 'Mo' Dewji**



# SIMBA, YANGA NA DABI YA UFUNDI, MBINU BILA UBABE



Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (katikati), akimiliki mpira dhidi ya Kiungo wa Yanga, Khalid Aucho (kushoto) na beki Shomari Kibwana kwenye mechi ya Ligi Kuu wakati timu hizo zikitoka suluhu Uwanja wa Mkapa juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Adam Fungamwango**

DAKIKA 90 zilikamilika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi kwa wababe wa soka nchini, Simba na Yanga kugawana pointi moja kwa sare ya bila kufungana. Ni matokeo ambayo si wengi walitarajia, hasa kutokana na kile kilichokuwa kikizungumzwa na wachambuzi wa soka na mashabiki kabla ya mechi yenyewe.

Ni mechi iliyoonekana nyepesi kwa Yanga kushinda na si Simba. Ni sare ambayo imeonekana kuwaridhisha wanachama na mashabiki wa Simba zaidi kuliko wa Yanga.

Baada ya mechi kumalizika, baadhi ya mashabiki wa Yanga walionekana hawaamini kilichotokea kwa sababu kikosi walichonacho sasa walijua ndiyo wakati wao si wa kuifunga Simba tu, lakini kuwafunga mabao mengi. Wengine walionekana kushika vichwa, wengine wakisimama na kushindwa kutoka uwanjani.

Hali ilikuwa tofauti na wenzao wa Simba kwani wanavyoonekana walikuwa tayari kuyapokea matokeo ya aina yoyote ile. Bado mashabiki wengi wa Simba wanaamini kikosi chao hakichezi soka kama la msimu uliopita, pia hakijakamilika kwa baadhi ya wachezaji kuwa majeruhi kama Thadeo Lwanga na Chris Mugalu, hivyo hawakuwa na uhakika sana wa moja kwa moja na ushindi, lakini walijipa moyo tu kwa sababu mechi ya 'dabi' huwa mara nyingi haina mwenyewe. Na kweli ndivyo ilivyokuwa.

**Mechi isiyokuwa rafu, ubabe**

Baada ya miaka mingi, mashabiki wa soka waliokuwapo uwanjani na waliokuwa wakiangalia kwenye televisheni, walishuhudia mechi isiyokuwa na matumizi makubwa ya nguvu kama vile rafu nyingi na ubabe.

Kwa miaka kadhaa nyuma, mechi za Simba na Yanga hutawaliwa na matumizi makubwa ya nguvu, wachezaji kuchezeana 'undava', kiasi kwamba hata mechi ikiisha kunakuwa na video fupi nyingi za matukio ya kuchezeana ubabe ambazo zinazoonekana na mwamuzi na zisizoonekana.

Ni mechi ambayo wachezaji wa pande zote mbili waliamua kuweka mpira chini na kutandaza kabumbu, na hii huenda inachangizwa zaidi na uwezo wa wachezaji wengi wa kigeni ambao wamekuja kuifanya 'dabi' kuwa burudani zaidi na si kukamiana na kuumizana kama ilivyokuwa huko nyuma.

**Mbinu za Pablo balaa**

Mashabiki waliokuwa wanaangalia mpira uwanjani na hata kwenye televisheni walikuwa wanapata burudani ya kuona mbinu za makocha ambazo walikuwa wamezipandikiza kwa wachezaji wao.

Kuwapo pia kwa makocha wa kigeni wenye uwezo wa hali ya juu, kumeifanya pia mechi ya Simba na Yanga kuwa ya kiufundi na mbinu zaidi, badala ya 'miguvu' na butuabutua tulizokuwa tukizishuhudia miaka kadhaa nyuma.

Pablo Franco, Kocha Mkuu wa Simba alionekana kuingia kwa kuiheshimu Yanga, baada ya kuisoma na kuifuatilia jinsi inavyocheza.

Nadhani alijua Yanga ni wazuri na wana nguvu zaidi dakika 30 za mwanzo na wamekuwa wakiifunga Simba mabao kwenye dakika kuanzia ya 10 hadi ya 15 na huwa halirudi, hivyo hawakufunguka kabisa kipindi chote cha kwanza.

Ni kipindi ambacho Simba ilifanya shambulizi moja tu, lakini kipindi cha pili ndipo ilipokuja juu na kulitia msukosuko lango la Yanga.

Pia alijua Yanga inaweza kuingia kwenye mtego wa kufanya kama Red Arrows walivyofanya kwenye mechi ya marudiano ya kushambulia kupitia kwa Mohamed Hussein, hivyo kumweka Sadio Kanoute asaidie eneo hilo na kweli ikawa hivyo na akafanikiwa kudhibiti hali hiyo.

**Nabi ashtukia janja ya Pablo**

Wakati wanachama wengi wa Yanga na mashabiki wao wakidhani Simba haiko vizuri hivyo wanaweza kupata ushindi kirahisi, kwenye akili ya Nasreddine Nabi, Kocha Mkuu wa Yanga haikuwa hivyo.

Alijua Simba bado ni timu nzuri na ina wachezaji wazuri wanaoweza kuamua mechi, akawakataza kabisa Djuma Shaban na Kibwana Shomari kupanda mbele kwa sababu wapinzani wao walikuwa na mawinga wenye kasi na matata kama Hassan Dilunga na Bernard Morrison. Ndiyo maana mabeki hao wa pembeni hakuonekana kwenda mbele kuleta kashikashi zao ambazo zimezoeleka.

**Simba ilinufaika na 'sub'**

Simba ilinufaika zaidi na wachezaji wa akiba kuliko Yanga kwenye mechi ya juzi. Hii inaendelea kuonyesha kuwa 'Wekundu wa Msimbazi' hao wana wachezaji wazuri zaidi wanaokaa benchi kuliko wapinzani wao.

Ndiyo maana haikushangaza Yanga ilipobadilisha wachezaji wawili tu ambao ni Farid Mussa na Heritier Makambo walioingia badala ya Fiston Mayele na Jesus Moloko na hawakuwa na msaada sana kwenye timu.


Simba iliwaingiza John Bocco, Rally Bwalya na Yusuph Mhilu kuchukua nafasi za Meddie Kagere, Kibu Denis na Morrison, mabadiliko ambayo yalileta shida kwenye lango la Yanga.

**Ni sare ya 32**

Imekuwa ni sare ya 32 kwa timu hizo tangu kukutana kwenye mechi za Ligi Kuu tangu ianzishwe mwaka 1965, bila kuhesabu michuano mingine.

Simba na Yanga zimetimiza mechi ya 102 za Ligi Kuu, Yanga ikishinda mara 39, Simba ikipata ushindi mara 31.

**JE, WAJUA?**



BAO la kusawazisha Zlatan Ibrahimovic aliloifungia AC Milan wakati ikitoka sare ya 1-1 ugenini dhidi ya Udinese juzi, linamfanya kuwa mchezaji wa tatu katika karne ya 21 kufikisha mabao 300 katika ligi tano bora Ulaya, Italia- Serie A, Hispania - La Liga, England - Premier League, Ujerumani - Bundesliga na Ufaransa - Ligue 1, hivyo kuwa nyuma ya Cristiano Ronaldo (483) na Lionel Messi (475). Mabao hayo ni kwenye Ligi Kuu pekee.







Mkurugenzi wa Shule ya Msingi Ilakoze Nzunguni jijini Dodoma, Olipa Mkuyu, akizungumza na wazazi wa wanafunzi (hawapo pichani) kwenye mahafali ya darasa la awali (Pre- Standard One) iliyofanyika mwishoni mwa wiki. Watatu kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shule, Evarist Msakila. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Maduka ya dawa marufuku kuuza bila cheti cha daktari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MSAJILI wa Baraza la Famasi Tanzania, Elizabeth Shekalaghe, amepiga marufuku wamiliki wa maduka ya dawa kuuza dawa kwa mtu asiyekuwa na cheti cha daktari.

Shekalaghe, alitangaza marufuku hiyo juzi jijini Dodoma alipokuwa akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari kuhusu matumizi holela ya dawa.

Alisema, wananchi wanapaswa kuelewa kuwa dawa ni sumu hivyo hawanabudi kuzingatia matumizi yake kwa mujibu wa melekezo ya wataalamu wa afya.

"Ni marufuku kwa wamiliki wa maduka ya dawa kuuza dawa kwa mtu bila kuwa na cheti cha daktari, lakini mwananchi hapaswi kununua dawa bila kuwa na cheti cha daktari. "Kwa yeyote atakaye bainika kuuza dawa bila kuwa na cheti cha daktari adhabu yake ipo wazi ni faini ya Sh. milioni tano au kifungo cha miezi 12," alisema Shekalaghe.

Aidha, alisema wananchi wanapaswa kuelewa kuwa kabla ya kununua dawa wanatakiwa kufanya vipimo kwa daktari na kupatiwa cheti kwa ajili ya kununua dawa.

"Wananchi wanatakiwa kuacha tabia hii ya kununua dawa katika maduka ya dawa bila kuwa na cheti cha daktari...wengi hivi sasa wananunua dawa na kutumia kiholela hali ambayo inachangia kuleta usugu wa magonjwa mbalimbali mwilini," alisema.

Alisema pamoja na kununua dawa bila cheti cha daktari, lakini wamekuwa wakinunua dawa chini ya dozi zinazostahili kwa ugonjwa husika.

"Unakuta mtu anaumwa ananunua vidonge viwili ambavyo haviwezi kumsaidia kupona na akiendelea kuumwa ananunua tena vingine viwili hali ambayo inatengeneza usugu wa magonjwa," alisema. Vilevile, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kununua dawa katika maduka ambayo hayajasajiliwa kwa ajili ya utoaji wa dawa. "Matumizi sahihi ya dawa yanajumuisha mgonjwa kufanyiwa uchunguzi wa kina, kuandikiwa na kupewa dawa inayostahili kulingana na hali ya ugonjwa alionao, kutumia kiasi sahihi kwa njia sahihi na kwa muda mwafaka kama alivyoelekezwa na mtaalamu wa afya, matumizi sahihi yanajumuisha pia jinsi dawa inavyotakiwa kuhifadhiwa kwa kipindi chote cha matibabu, alisema.

Kadhalika, alisema faida za matumizi sahihi ya dawa ikitumika kiusahihi itapunguza uwezekano wa kujenga usugu kwa vimelea vya magonjwa, kupunguza madhara, maudhi ya dawa na kupunguza gharama za matibabu kwa mgonjwa na serikali.

"Faida nyingine za matumizi sahihi ya dawa husaidia kupunguza uwezekano wa kupata magonjwa yatokanayo na utumiaji sugu wa dawa, huboresha afya ya mtumiaji wa dawa na hivyo kupona kwa wakati pamoja na kujenga imani na mifumo ya kutolea huduma za afya," alisema.

# Wauguzi, wakunga wakumbushwa wajibu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Uuguzi na Ukunga Tanzania limewata wataalamu wa afya kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, taratibu na miongozo ya taaluma zao.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza hilo, Prof. Lilian Masele, kwenye mahafali ya tatu ya wauguzi na wakunga iliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema wauguzi na wakunga wanatakiwa kuhakikisha wanatoa huduma bora ya afya na kwa kutumia lugha nzuri ili kuonyesha upendo kwa wateja wanao wahudumia kila siku.

Hata hivyo, alisema wahitimu hao wanatakiwa wakawe waadilifu katika kutekeleza majukumu yao ili kuweza kusaidia serikali na jamii kwa ujumla.

"Serikali yetu inahakikisha inatoa kipaumbele katika sekta ya afya hasa kwa kupunguza vifo vya mama na mtoto pamoja na magonjwa yasiyoambukiza na ya kuambukiza.

"Kwa hiyo ni jukumu lenu kwenda kufanya kazi kwa utii, weledi, maadili na unyenyekevu ili kupunguza maneno yanayosemwa juu ya wahudumu wa afya mhakikishe mnakuwa waadilifu na kuipenda kazi yenu lazima malalamiko yataisha,"alisema.

Alisema wauguzi wako zaidi ya asilimia 70 nchini katika kada ya afya, lakini huduma zinazotolewa haziridhishi hivyo kila mhudumu akiwa na upendo na kuipenda kazi yake huduma za afya zitakuwa bora zaidi ya sasa.

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga, Agness Mtawa, alisema kuwa lengo ni kuhakikisha kada hiyo inazingatia sheria na taratibu za kazi.

Alisema wauguzi na wakunga wanatakiwa kutoa huduma kwa kiwango ambacho kinatakiwa kwa kufuata miongozo ya kazi.

Vilevile, alisema wanasiasa wamekuwa wakiingilia taaluma hiyo jambo ambalo baraza limekuwa likifuatilia kwa ukaribu ili kutatua mogogoro mbalimbali ambayo imekuwa ikijitokeza.

"Licha ya kuwa na changamoto baraza linaangalia namna ya kupunguza na kukabiliana na malalamiko hayo ambayo yanatolewa na wateja wetu ambao ni wagonjwa," alieleza Mtawa.

Jumla ya waauguzi na wakunga 1,224 walikula kiapo katika mahafali hiyo na kupewa vyeti vya usajili na leseni ambavyo watavitumia kwenda kutoa huduma katika maeneo mbalimbali nchini.

# 'Jengeni utamaduni wa kujiwekea akiba'

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Kamishna wa Idara ya Maendeleo ya Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha na Mipango, Dionisia Mjema, amewataka Watanzania kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba kwa ajili ya kukuza uchumi wao.

Aidha, amevitaka vyama vya akiba na mikopo kutekeleza matakwa ya kisheria ya utoaji huduma pamoja na kutatua matatizo ya wanachama wao na kuimarisha mifumo ya utoaji huduma.

Mjema alitoa ushauri huo alipomwakilisha Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kwenye ufunguzi wa mkutano mkuu wa nane wa Chama cha Akiba na Mikopo (SACCOS) cha Hazina kilichofanyika jijini hapa juzi.

Aliwataka wananchi kujenga tabia ya kujiwekea akiba ya fedha kwa ajili ya maisha yao na vizazi vyao vijavyo.

"Wananchi tujenge tabia na utamaduni wa kujiwekea akiba kwenye maisha yetu hiyo ndio njia pekee ya kuimarisha uchumi wetu kwa maisha haya na yajayo," alisema.

Kadhalika, aliwataka kuongeza ubunifu katika utoaji huduma na kuhamasishana katika kuongeza hisa na kuweka mipango ya kuongeza wanachama wapya.

Aidha, aliwataka wanachama hao kutumia vizuri fedha za mikopo watakazopata kutoka mfuko wao na kurudisha kwa wakati ili wengine waweze kukopa.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Hazina, Aliko Mwaiteleke, alisema ushirika huo ulianzishwa mwaka 1972 ukiwa na wanachama 100, lakini hadi kufikia sasa kuna wanachama takribani 5,624.

Alibainisha kuwa idadi hiyo ni kutoka katika mafungu 282 kutoka Tanzania Bara na mapango wa Saccos ni kuwafikia wanachama zaidi.

Mwaiteleke, alisema kuwa chama chao kinamtaji wa Sh. bilioni 1.2 na kimeshatoa mikopo yenye thamani ya Sh. biloini 14.1 na thamani ya SACCOS yao ni Sh. bilioni 15.1.

Pia alisema mkutano huo umehudhuriwa na wawakilishi wa Hazina na saccos wapatao 300 kutoka wizara mbalimbali za serikali kwa lengo la kupanga na kujadiliana mafanikio na matatizo kwa mwaka 2021 na utakuwa wa siku mbili.

Kadhalika, alisema wanatarajia kupunguza riba ya mikopo kwa wanachama wake kutoka asilimia 12 hadi 11 ili kuwavutia wanachama wapya kujiunga na chama hicho.

Aliongeza kuwa wanatarajia kuongeza kiwango cha mikopo ya dharura kwa wanachama wao kutoka Sh. milioni mbili hadi kufikia milioni tano.



## Mamilioni kujenga madarasa ya shule za msingi shikizi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imetoa shilingi milioni 80 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi shikizi zilizoko katika kijiji cha Nyalwela Kata ya Ilungu Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nyalwela, Teophanes Mgina, wakati akisoma taarifa ya ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa kwa shule shikizi mbili ambazo ni Kasongo na Loleza kwenye ziara ya Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini, Oran Njeza, kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya shule katika kata hiyo.

Mwalimu Mgina aliishukuru serikali kutoa shilingi milioni 40 kwa kila shule shikizi mbili anazozisimamia ikiwamo Loleza ambayo tayari ina watoto wa darasa la pili na vyumba viwili na ofisi ya walimu vilivyojengwa kwa nguvu za wananchi huku akishukuru kwa usajili wa Shule ya Msingi Isyonje.

"Kukamilika kwa ujenzi wa shule shikizi katika eneo letu kutasaidia kudahili wanafunzi wengi sambamba na watoto kusoma kwa furaha ili kutimiza ndoto zao," alisema Mwalimu Mgina.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Ilungu, Ibrahim Mwakasege, alimwomba mbunge huyo kuendelea kutatua kero mbalimbali ikiwamo umaliziaji hatua zilizosalia kwenye vyumba vya awali viwili.

Alisema hadi sasa vyumba vimejengwa na wananchi, lakini madarasa hayo hayana nafasi ya kutoa kero zao mbele ya mwakilishi wao huyo bungeni ikiwamo kilio cha maji na barabara ya njiapanda ya Nyalwela hadi Ngole.

Mbunge Njeza alisema serikali ilitoa fedha hizo kwa lengo la kuepusha mrundikano wa wanafunzi madarasani ikiwa ni hatua mojawapo ya kuepukana na magonjwa ya kuambukiza ikiwamo corona.

Akijibu hoja za wananchi wake wa Nyalwela, Njeza aliwataka wananchi wa kijiji hicho kutobweteka badala yake waendelee kujenga majengo mengine kuelekea kusajiliwa kwa shule hizo, mpango wa kujengwa kwa barabara yao kwa kuanza na kilomita tano kutoka njiapanda ya Nyalwela kwa kiwango cha changarawe ili ipitike kwa urahisi na kuhusu maji.

Aliongeza kuwa serikali ina mpango wa kujenga mradi wa maji kwa ajili ya Kata ya Ilungu.

Watoto wa Shule ya Msingi Nyalwela wengi wao wamekuwa wakisafiri kwa miguu kwa kilomita tano kutoka majumbani kwao kwenda na kurudi kufuata elimu katika shule mama ya msingi Nyalwela na hakuna chakula shuleni.

# Bil. 4/- kujenga jengo la upasuaji hospitali ya rufani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imetoa zaidi ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Ngwilo Mwakyusa, alisema jengo hilo la upasuaji linajumuisha vyumba sita, ofisi za wataalamu na chumba cha kutakasia vifaa tiba.

Dk. Mwakyusa alisema jengo linatajarajiwa kukamilika Desemba 31, mwaka huu na kwamba itasaidia kuondokana na msongamano wa wagonjwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya.

Aliongeza kuwa hospitali hiyo pia inaendelea na ujenzi wa jengo la huduma ya dharura ambalo linagharimu zaidi ya shilingi milioni 877.5 fedha ambazo zilitolewa na Benki ya Dunia na fedha za serikali kutoka vyanzo vyake vya ndani.

"Tunaishukuru serikali yetu kwa kutupatia mabilioni ya fedha kujenga miundombinu bora na ya kisasa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi tunatembea kifua mbele kwa sababu sasa hospitali yetu ya rufani ya Kanda ya Mbeya inaendelea kutoa huduma bora za matibabu," alisema Dk. Mwakyusa.

Aidha, Dk. Mwakyusa alisema wakati Tanzania bara inaadhimisha miaka 60 ya uhuru wake, yako mambo mengi ambayo hospitali hiyo inajivunia ikiwamo kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kuhifadhia gesi ambayo itaunganishwa kwenye vyumba vyote vya upasuaji na wadi za wazazi.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuondokana na matumizi ya mitungi ya gesi ya mitungi kama ilivyo kwa maeneo mengine ambapo hutumia gharama kubwa kuzalisha na kuhudumia.

Kuwapo kwa majengo hayo ni hatua nyingine muhimu katika kuboresha huduma za kibingwa ambazo zilikuwa hazipatikani kwenye hospitali hiyo ambazo sasa zinapatikana.



Mkuu wa Kitengo cha Bima wa Benki ya NMB, Martine Massawe, akimkabidhi cheti Mwenyekiti wa Matukio wa Taasisi ya Mbeya Family Group (MFG), Rose Mkisi, wakati wa Mkutano Mkuu wa mwaka uliofanyika jijini Dar es Salaam. Taasisi hiyo ya MFG imetimiza miaka mitatu tangu kuanzishwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CBE yashauriwa kujipanua mikoani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimetakiwa kuboresha elimu kwa kujenga vyuo katika mikoa mingine ikiwamo Iringa, Lindi na Zanzibar ili kupanua wigo na kuwafikia wananchi wengi, hivyo kufikia malengo ya serikali katika kusambaza elimu ya biashara na ujasiriamali.

Hayo yalisemwa juzi na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, wakati wa mahafali ya 56 ya CBE Ndaki ya Mbeya.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa biashara katika kujenga taifa, hivyo ili kupata wataalamu wengi katika nyanja hiyo lazima kuwapo vyuo vingi hapa nchini ili kuwafikia wananchi wengi.

Alisema hadi sasa zipo kampasi nne za Chuo hicho ikiwa ni Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya, hivyo inahitajika uwapo wa ndaki nyingine kama Iringa, Lindi na Zanzibar.

"Serikali inatoa msisitizo kuongeza wataalamu kwenye elimu ya biashara kwa ustawi wa Taifa na katika kufikia malengo ... lazima kuwapo na wigo mpana kwa kujenga vyuo maeneo mbalimbali ikiwamo Iringa, Lindi ambapo Mh.Waizri Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa ekari 100 kajenge chuo, lakini Zanzibar," alisema Kigahe.

Kigahe aliongeza kuwa amefurahishwa na mkakati uliopo wa kampeni ya ujenzi wa hosteli za wasichana katika kampeni maalumu ya kuchangia ujenzi huo na kuwaomba wadau kujitokeza kuunga juhudi hizo ili kumaliza changamoto kwenye chuo hicho ndaki ya Mbeya.

Pia aliwataka wanafunzi kutumia taaluma waliyoipata kubuni miradi itakayowasaidia wao kujikwamua kiuchumi na jamii kwa ujumla pamoja na kuonyesha uweledi katika majukumu yao.

Kwa upande wake, Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Emanuel Mjema, alisema pamoja na mafanikio kwa mwaka wa nane sasa tangu kuwapo kwa tawi hilo, lakini changamoto imekuwa kwa vijana wanaohitimu kutopata ajira rasmi na kujikuta wakijiingiza katika makundi ya wahalifu.

Aliongeza kuwa katika mkakati wao wanatarajia kuanzisha shahada ya elimu ya biashara kuanzia mwakani kutokana na ujenzi wa chuo kukamilika kwani tatizo la kutokuanza mapema ilikuwa ni kutokuwa na madarasa ya kutosha.

"Tangu 2013 kuwapo kwa kampasi hii tumeongeza idadi ya wanafunzi kutoka 44 hadi 947, lakini changamoto kubwa wahitimu wamekuwa wakikosa ajira rasmi na kujikuta wakiacha taaluma zao, tunatarajia mwakani kuanza kutoa elimu ngazi ya shahada baada ya kukamilika kwa ujenzi wa chuo mwakani," amesema Prof. Mjema.






Katibu Mkuu Kiongozi wa Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said (katikati), akizungumza na mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhusu mchango wa Sera ya Uchumi wa Bluu katika kikao kilichofanyika jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri akagua usafiri wa meli bandarini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Usafirishaji, Miundombinu na Mawasiliano, Rahma Kassim Ali, amefanya ziara ya kushtukiza katika Bandari ya Malindi Zanzibar kuangalia mwenendo wa usafirishaji wa meli za abiria zinazotoka Unguja kwenda Pemba.

Katika ziara hiyo juzi, alisema kipindi hiki cha mwisho wa mwaka abiria wanaosafiri huwa wengi na baadhi ya vyombo vya usafiri huzidisha abiria, jambo ambalo ni kinyume cha utaratibu.

Waziri Rahma alisema haridhishwi na hali ya watoto waliokuwamo katika meli hizo ambao idadi yao ni kubwa kuliko abiria watu wazima.

Alieleza kuwa amejionea abiria mtu mzima ameambatana na watoto zaidi ya watano, jambo ambalo ni hatari endapo itatokea ajali.

Aliwataka wamiliki wa vyombo vya usafiri baharini kuwa makini na kuhakikisha abiria wote wanakuwa na tiketi halali.

Aidha, waziri huyo aliwataka wazazi na walezi kuacha kuwapa watoto wao jamaa zao au jirani zao wanaosafiri ili kusafiri nao.

"Unamkuta abiria amechukua watoto zaidi ya watano ambao sio wake amepewa tu na ndugu au rafiki asafiri nao, jambo ambalo ni hatari," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Mamlaka ya Usafiri baharini hapo, Shekha Ame Muhammed, alisema kuwa mamlaka yake itahakikisha inasimamia safari za meli na boti za abiria zinazokwenda Pemba na Unguja ili kuhakikisha usalama wa abiria.

Alieleza kuwa endapo meli itazidisha abiria, hatua za kisheria zitachukuliwa.

Kwa upande wao wasafiri wanaotoka Unguja kwenda Pemba waliiomba serikali kutafuta usafiri wa meli ili kuondoa usumbufu wa usafiri kutoka Unga kwenda Pemba.

Waziri Rahma alikagua meli ya Ikram na Silink ambazo hufanya safari kati ya Unguja na Pemba.

# Rais Mwinyi aiagiza Wizara ya Habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameuagiza uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuharakisha uandaaji na kutoa sera ya lugha pamoja na kuweka kanuni zitakazosimamia uandishi wa kazi za vitabu vya Kiswahili, ili kuilinda lugha dhidi ya upotoshaji.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alieleza hayo kupitia hotuba aliosoma kwa niaba ya Rais Dk. Mwinyi katika ufunguzi wa kongamano la tano la Kiswahili la kimataifa lililofanyika Zanzibar.

Alieleza kuwa katika siku za karibuni kumekuwa na wimbi kubwa la uandishi wa vitabu vya lugha ya Kiswahili ambavyo baadhi yao kutopita katika mamlaka rasmi zinazosimamia lugha zikiwamo BAKITA na BAKIZA.

Hemed alisema hali hiyo ya kukiukwa kwa taratibu kwa namna moja ama nyengine husababisha kukiuka miiko na desturi za kiutamaduni.

Alieleza hatua hiyo haina lengo la kuwavicha na kuwakwaza waandishi chipukizi, ila inalenga la kuwapitisha waandishi hao katika njia sahihi ya kuendeleza azma yao ya kuwafinyanga kuwa waandishi nguli kama wale waliowatangulia.

Aidha, Makamu wa Pili wa Rais alisema serikali zote mbili zinaendelea kufanya juhudi za kukiendeleza Kiswahili katika kuifanya iweze kutumika kikamilifu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (SADC), Umoja wa Afrika (AU), na Umoja wa Mataifa (UN).

Katika hatua nyingine, Hemed alitoa wito kwa waandishi wengine kuiga mfano wa Profesa Abdurazak Salim kwa lengo la kuchangia maendeleo ya utamaduni wa mswahili ikiwamo lugha ya Kiswahili.

Pia, alikitaka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kiandae mikakati ya kuimarisha mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa kuwa na programu maalum ya kufundisha lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za kigeni ili kuzalisha wataalamu wengi wa kutafsiri na ukalimani wenye viwango vya kimataifa.

"BAKIZA kwa upande wenu mna wajibu wa kuhakikisha kuwa Zanzibar inaendelea kuwa chemuchemu ya kuzalisha waandishi bora wa Isimu na Fasihi ya Kiswahili," alisema Makamu wa Pili wa Rais.

Alilitaka BAKIZA kuendelea kuhamasisha waandishi chipukizi na kuwasimamia sambamba na kujenga ushirikiano wa karibu ili kuendelea kuwaibua waandishi wapya wenye vipaji miongoni mwa vijana husuani waliopo shuleni.

Naye Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema mabaraza ya Kiswahili yaliopo katika ukanda wa Afrika Mashariki yamesaidia kukitangaza Kiswahili katika mikutano ya kitaifa na kimataifa.

Tabia alieleza kwamba Kiswahili kimesaidia kwa kiasi kikubwa katika harakati za ukombozi wa Bara la Afrika, ambapo lugha hiyo imekuwa ikitumiwa katika mawasiliano kwa ajili ya kufanikisha harakati hizo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa BAKIZA, Saade Said Mbarouk, alisema kongamano hilo lina lengo la kutathmini mchango wa TEHAMA kwa maendeleo ya Kiswahili.

Saade alisema pamoja na mafanikio yaliofikiwa na Baraza hilo, lakini linakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa nyenzo kwa ajili ya ukamilishaji wa Kamusi la Kiswahili linaloandaliwa na baraza hilo.

Aliiomba serikali iwasisitize wakuu wa taasisi mbalimbali za serikali kutumia lugha ya Kiswahili katika utoaji wa taarifa au kutoa matangazo kutokana na jamii kubwa inayofika katika taasisi hizo kupata huduma inatumia lugha ya Kiswahili.

Akitoa Salamu za Chama cha Afrika Mashariki, Henry Indeed, alisema kuna haja kwa watu wa Afrika Mashariki kukitumia Kiswahili kama bidhaa kwa kuiuza ili ilishe Afrika Mashariki.

# 'TEHAMA itapaisha uchumi wa bluu'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa TEHAMA katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amani, Omar Said Ali, amesema kuwa hivi sasa serikali imeingia katika uchumi wa bluu na teknolojia ya TEHAMA ikifanya kazi yake, maendeleo makubwa yatapatikana katika uchumi wa Zanzibar.

Mkurugenzi huyo alisema vijana wanatakiwa kufahamu kuwa suala la ubunifu na utafiti lina umuhimu wake kwa Zanzibar, hivyo kuna wajibu mkubwa vijana kujitoa na kuwa tayari katika kujifunza TEHAMA.

Aliyasema hayo jijini Zanzibar wakati akifungua maonyesha ya Chuo cha Taifa (SUZA) kuhusu teknolojia ya habari ya siku ya ubunifu duniani.

Alisema ubunifu ni jambo muhimu katika hatua za maendeleo na serikali imetoa punguzo kwa vifaa vya fani hiyo.

Alisema hivi sasa katika dunia watu wanakwenda katika mfumo wa teknolojia, mfumo ambao umetengeneza fursa kubwa kwa vijana kuajiriwa na kujiajiri.

Naye Makamu Mwenyekiti wa SUZA, Prof. Mohd Makame Haji, alisema maonyesho hayo ya kwanza kufanywa na chuo hicho, lakini yanaonyesha mwanga wa maendeleo ndani ya chuo hicho.

Alisema mpango wa chuo hicho ni kufanyika kila mwaka kadri hali ya fedha itakapo ruhusu ili kutoa nafasi kwa vijana kuonyesha uwezo wao wa ubunifu ili kuwajenga kuwa wataalamu.

Kwa upande wake mwalimu wa somo la TEHAMA SUZA, Dk. Abuubakari Diwani Bakari, alisema hivi sasa dunia inakwenda na teknolojia, hivyo wanafunzi wanatakiwa kufahamu TEHAMA na maendeleo yake.

Alisema iwapo wanafunzi watakuwa na uthubutu wa ubunifu hasa katika mambo ya teknolojia ya habari, watapata nafasi ya kuajiriwa na kujiajiri.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# VACANCIES ANNOUNCEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is making reforms in its structure, internal operations and staffing to accommodate business needs. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following vacant positions:

**1. POSITION: TRAFFIC LIAISON OFFICER (1 POST)**

**1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Bachelor Degree or relevant Aviation related Diploma/Certificate from a recognized Training Institution
- Proven relevant working experience of not less than 3 in Airport Ground Operations
- Must be computer literate
- Background in Air Transport Management and possession of IATA/UFTAA Diploma or equivalent will be an added advantage
- Experience in delivering service in demanding consumer environment
- Fluency in appropriate foreign languages is an added advantage

**1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Supervise and ensure efficient and effective check in and boarding of passengers in compliance with carrier's policy/ procedures and customer expectations
- Supervise baggage handling and prepare weekly baggage handling report.
  Liaise with the GHA to ensure lost baggage is communicated, traced, and delivered to affected passenger
- Audit, review and report on service delivery to monitor compliance on SLAS's availed to GHA
- Strict control of excess baggage collection and remittance
- Record all flight movements as per company requirement
- Any other duties as may be assigned by your supervisor
- Ensure the application of the Ground Handling Manual, ATCL rules and Regulations as well as other regulatory authorities' guidance amid operations
- Ensure Operations are performed safely and on time in line with applicable regulations and guidance
- Timely report incidents, accidents, delays, disruptions as observed during operations for further analysis and investigation
- Complete investigation as assigned and share findings within the time frame allocated
- Plan the resources to ensure that every shift and flight is sufficiently covered
- Make decision over the ground operations after consultation with other parties and approval from the manager or as per the written procedure
- Act as a link between ATCL and other service providers.
- Deliver on the OTP and Safety KPIs for ATCL

**2. POSITION: CARGO SALES OFFICER (2 POSTS)**

**2.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORKING EXPERIENCE:**

- Must have a Degree in Business Administration/Air Transport Management or its equivalent from a recognized institution
- Must have two years (2) working experience in sales in highly competitive business environment
- Background in aviation industry and/or possession of aviation related certification will be an added advantage

**2.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES:**

- Coordinate and supervise cargo sales activities from all stations
- Verify and sign cargo damage reports.
- Oversee Ramp staff are advised on the cargo to be uplifted on each flight
- Supervise the Handling agent (at some stations) performs all activities as per TC recommended procedures.
- Prepare periodical reports
- Assist in preparation of budget inputs
- Handle general cargo and Post Office mail bags at point of origin
- Check incoming cargo and mail against the cargo manifest
- prepare arrival advices for all received cargo as per cargo manifest
- Accept cargo from shippers and prepare for carriage all shipments from agents.
- Investigate and respond to customer complaints and restore customer confidence where there has been service failure
- Handle acceptance of coffins, perishables and courier shipments
- Monitor market trends, competitors' activities and special deals and recommend strategies and marketing activities to counter the competition
- Maintain sales call records and statistics (rates, volumes, revenues, yield, seasonal variations) and produce periodic performance reports on existing accounts, including recommendations to maximise client support
- Forward invoicing particulars to Finance department.
- Manifest all shipments accepted

**3. POSITION: SALES EXECUTIVE (1 POST)**

**3.1 MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORKING EXPERIENCE**

- Must have Bachelors' Degree preferably in Commerce, Business Administration or relevant discipline.
- Must have at least three years' experience in airline sales working directly for an airline, or within a Travel Agency will be an added advantage
- Must be computer literate.
- A background in Air Transport Management and possession of aviation related certification will be an added advantage

**3.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Ensure that set revenue targets are achieved within prescribed time limits and contribute to total area achievement.
- Enhance relationships with the entire Travel Trade in the assigned territory
- Contributes to the formulation and implementation of ATCL sales strategy to maximise short- and long-term revenue opportunities, reduce cost of sales and generating channel shift where appropriate
- Resolve operational and reservations issues from travel agents and other corporate clients
- Develops tactical sales and marketing activity in support of sales opportunities in both Trade Partners and Corporate market place
- Analyze business environment to facilitate timely response to developing market trends to maximise on opportunities that arise and minimise adverse impact on company sales.
- Monitor competitor activities, evaluate recommend competitive strategy and pricing levels to deliver expected yield, margin and revenue targets
- Ensure that all travel agents and corporates are prioritised, regularly visited and professionally handled by the sales team to increase revenue and gain market share.
- Provide input and participate in the identification and progress of new business opportunities for revenue growth (through Agents Incentives/ Corporate agreements /partnerships/ Major Events & Conference Organisers etc).

**4. POSITION: MARKETING OFFICER (1 POST)**

**4.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATION AND WORKING EXPERIENCE**

- Must have at least a Bachelor's Degree in Marketing, Business Administration/Air Transport Management or its equivalent from a recognized institution.
- Must have at least 3 years working experience in a similar function
- Possession of a Master Degree/Aviation related certification and/or background in aviation will be an added advantage

**4.2 DUTIES AND RESPONSIBILITIES:**

- Identify marketing opportunities by identifying consumer requirements; defining market, and competitor's strengths and weaknesses; forecasting projected business; and establishing targeted market share
- Prepare the marketing plan/activities to actively promote brand awareness
- Lead the communication plan, including traditional media activation as well digital tactical strategies
- Maximize the image and the reputation of the transportation group by establishing credibility and maintaining good working relationships with customers' management team and the aviation community
- Oversee the company's marketing budget
- Coach and develop members of marketing team as required
- Monitor and report effectiveness of marketing communications
- Develop and implement effective promotion and trade incentive programs

**5. POSITION: SENIOR ACCOUNTANT (3 POSTS)**

**5.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE**

- Must have Bachelor's degree in Accounting, Finance or relevant qualifications from a recognized institution
- Must have at least five (5) years working experience
- Must have relevant certification ie CPA or ACCA) and registered with NBAA
- Experience in airline accounting (BSP and ICH transactions) will be preferred.
- Advanced MS Excel skills including VLOOKUP and pivot tables will be preferred

**5.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Verify, allocate, post and reconcile accounts payable, receivable, revenue, fixed assets and inventory.
- Produce weekly and monthly report of revenue, payable, receivable, fixed assets and inventory
- Summarize and analyses financial information
- Participate in financial standards setting and forecast process
- Prepare financial statements timely and submit to finance manager for review
- Design the frame-work of cost and financial accounts and prepare reports for routine financial and operational decision-making
- Prepare routine reports as well as reports for long-term decision-making and forward to Finance manager to take corrective action at the right time.
- Prepare management report timely and submit to Finance manager for review
- Ensure Compliance with tax related issues, tax audits and tax returns
- Provide support to internal and external audit assignments assign
- Prepare and update cash flows projection
- Support month-end and year-end close process
- Provide input into department's goal setting process
- Supervise, train and coach Assistant accountants reporting to you.
- Participate in department's goal setting process
- Advise Finance Manager on financial related issues, internal controls and reporting.
- Review and recommend modifications to accounting systems and procedures
- Develop and document business processes and accounting policies to maintain and strengthen internal controls
- Ensure compliance with GAAP principles, IASs, IFRSs and IPSAs.

**6. POSITION: ACCOUNTANT GRADE 1 (2 POSTS)**

**6.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE**

- Must have Bachelor Degree in Accounting, Finance, Banking or its equivalent from recognized academic institutions
- Must have Professional Qualifications (CPA, ACCA or equivalent)
- Must have at least three (3) years working experience in a competitive business environment
- Knowledge in the accounting information system, experience in inventory accounting and relevant airline experience will be an added advantage

**6.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Record inventories (spare parts) in the accounting system
- Reclassify inventories to match with company chart of accounts
- Reconcile accounting records against store physical inventories
- Reconcile accounting records against procurement records
- Undergo monthly inventories stock taking, reconciliation, and valuation
- Advise Finance manager on the provision of obsolete stocks and pass appropriate adjustments
- Analyze business risks associated with inventory management and proposed remedial actions to financial manager
- Support internal and external auditing on inventory accounting
- Comply with financial regulations and accounting standard in reporting, classifying, and disclosure of inventory accounting
- Verify and process invoices into the system
- Perform monthly suppliers' reconciliation
- Review invoices and requisitions for satisfactory payment approval
- Calculate, post business transactions, process invoices, verify financial data for use in maintaining accounts payable records, and provide other clerical support necessary to pay the obligations of the organization
- Maintain copies of vouchers, invoices or correspondence necessary for files
- Prepare vouchers listing invoice number, date, vendor address, item description, amounts and coding per accounting policies and procedures
- Keeping track of all payments and expenditures, including payroll, purchase orders, invoices, statements, etc.
- Maintaining historical records by handling accruals and prepayments
- Paying vendors by scheduling pay checks and ensuring payment is received for outstanding credit; generally responding to all vendor enquiries regarding finance
- Perform any other duties may be assigned by the supervisor.

**7. POSITION: ASSISTANT ACCOUNTANT (1 POST)**

**7.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE**

- Holder of Bachelor Degree in Accountancy, Finance, Commerce/Business Administration (majoring in Accountancy or Finance) or equivalent qualifications from a recognized institution.
- Must have at least two (2) years working experience in a competitive business environment
- Must be Computer literate
- Knowledge in the accounting information system, experience in inventory accounting and relevant airline experience will be an added advantage

**7.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Receives cash and cheques, keeps and makes payments to authorized persons against approved documents;
- Collect and keeps petty cash for payment and for other official use
- Prepare petty cash, cash receipts and maintains petty cash book and passes journal entries
- Prepare and maintain accounting records as per Company Financial regulation
- Ensure that the Agency's cash and cheques are duly deposited and recommends the best way of handling cash to and from the bank
- Prepare payments by verifying documentation, and requesting disbursements;
- Document financial transactions by entering account information
- Post suppliers' invoices and prepare payment vouchers
- Prepare revenue accounts schedules and reconciliation
- Prepare monthly payroll slips for each employee, and keeping records and pay- roll registers
- Remit net salaries to the employee 'respective banks Accounts or preparations of authorized lists for those employees to be paid in cash
- Maintain the employees' ledger for staff advances, loans and duty travel imprests
- Monitor, process and reconcile all inter-billing sales
- Preparation of various accounting schedules as directed by supervisor and
- Perform any other official duty as may be assigned by your supervisor.

**8. EMPLOYMENT TERMS:**

Five (5) years contract with remuneration and fringe benefits as per ATCL Scales and Incentive Scheme

**9. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following: -

i. A detailed curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school), birth certificate and other relevant certificates/licenses. **Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)**
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

**10. CLOSING DATES:**
The application letters should reach the undersigned within fourteen (14) days from the first date of this announcement.

The application letters should be directed to the following address: -

**MANAGING DIRECTOR AND CHIEF EXECUTIVE OFFICER,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. BOX 543,**
**DAR ES SALAAM.**

**13th December, 2021**

# Serikali yaonyeshwa siri wahitimu kujiajiri

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

SERIKALI imeombwa kuvibana vyuo vikuu nchini kuweka mitaala itakayosaidia wahitimu kujiajiri wenyewe au kuendana na uhitaji wa soko la ajira.

Imebainishwa kuwa hatua hiyo itawafanya wasitegemee ajira za serikali pekee.

Hatua hiyo inatokana na mitaala inayotumika kufundishia katika vyuo vikuu nchini kutajwa kuwa ni miongoni mwa sababu ya wahitimu wengi kushindwa kujiajiri na kuwafanya wasubiri ajira za serikali.

Ombi hilo limewasilishwa na Fatma Aziz, mwanafunzi wa mwaka wa tatu, akichukua shahada ya Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Biashara, katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi kuu ya Morogoro.

Aliwasilisha ombi kwenye mkutano wa hitimisho la mradi wa kuleta mabadiliko katika sekta ya ajira kwa manufaa ya Jamii Afrika Mashariki (TESCEA) katika vyuo vikuu vinne vya Tanzania na Uganda, kutafuta suluhu kwa wahitimu kukosa ufanisi.

Mkutano huo wa hitimisho pia ulioshirikisha watumishi wa serikali, waajiri, sekta binafsi, wanafunzi na waadhiri kujadili changamoto mbalimbali za ajira na kupeana miongozo na mikakati ya kuboresha ufundishaji kwa ajili ya kusaidia wanafunzi.

Alisema wahitimu wa vyuo vikuu ni kati ya wanaobeba taswira ya uhalisia katika mfumo wa elimu nchini na lawama zimekuwa zikielekezwa kwao wakioonekana wengi wao hawaajiriki kwa kuwa hawana ujuzi wala uwezo wa kujiajiri.

Mwanafunzi huyo ambaye alizungumza kwa niaba ya wenzake walioshiriki katika mradi huo, alisema wamebaini kuwa kiini kikuu ni mfumo wa elimu yenyewe kwani mitaala inayotumika haiendani na uhalisia, na kwamba haimwandai mwanafunzi anapohitimu kujiajiri hata anapokosa kazi ya serikali.

Julieth Kalalu wa chuo hicho ambaye nae alishiriki katika mradi huo, alisema ipo haja kwa serikali sasa kuja na mpango wa haraka, kufanyia maboresho mfuno wa elimu ikiwamo kuhakikisha vyuo vikuu vinaweka mitaala itakayosaidia wanafunzi kujiajiri na kuwa na ujuzi badala ya kutegemea ajira ambazo kwa sasa zimekuwa ni ngumu.

Mhadhiri kutoka Mzumbe, Dk. Musali Milanzi, alisema umefika wakati sasa kubadili mfumo wa ufundishaji utakaowafanya wahitimu kujua vitu kulingana na elimu wanayofundishwa darasani na badala yake mbinu za ufundishaji lazima ziwajenge katika ubunifu, maarifa na halisia kuwawezesha kujiajiri wenyewe.

Kwa upande wake Mratibu Mkuu wa Mradi wa TESCEA, Dk. Prepetua Kalimasi, alisema mradi ulihusisha waajiri kutambua maarifa na ujuzi ili kuja kusaidia mitaala ya vyuo vikuu ili kuboresha ujuzi mahiri kwa wahadhiri katika vyuo hivyo vilivyoshiriki katika mradi huo.

**Ombi hilo limewasilishwa na Fatma Aziz, mwanafunzi wa mwaka wa tatu, akichukua shahada ya Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Biashara, katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi kuu ya Morogoro.**

# Maelfu ya watalii walivyotembelea maeneo ya kihistoria Bagamoyo

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

WATALII 368,727 wametembelea katika Kituo cha Kaole na mji mkongwe Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani kwa kipindi cha miaka kumi.

Hayo yameelezwa na Mhifadhi Mali Kale Kaole Wilaya ya Bagamoyo, Kelvin Fela, alipokuwa akitoa taarifa za uhifadhi wa vituo vya Kaole na Mji mkongwe kwa kipindi cha miaka kumi.

Fela alibainisha hayo wakati wa mwendelezo wa maaadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru yaliyofanyika Kaole Bagamoyo ambayo yaliandaliwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Mashariki.

Akitoa taarifa hiyo alieleza kuwa katika kipindi hicho cha miaka kumi watalii 249,332, walitembelea kituo cha Kaole na 119,395 walitembelea kituo cha mji Mkongwe.

Alisema kati ya wageni mashuhuri waliotembelea vituo hivyo yumo Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Rwanda, Paul Kagame na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyata.

Aidha, Fela alielezea vikwazo wanavyokumbana navyo kuwa ni pamoja na migogoro ya ardhi na mipaka, wizi wa mali kale uchakavu wa majengo ya kale na baadhi ya wananchi kutotambua umuhimu wa mali kale.

Mhifadhi huyo alisema zipo hatua zimechukuliwa kukabiliana na vikwazo hivyo kuwa ni baadhi ya wahifadhi kupatiwa mafunzo ya kijeshi kuimarisha ulinzi na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusiana na umuhimu wa mali kale.

Akizungumzia kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Malboard Kapinga, alitoa maelekezo kwa TFS kutangaza vivutio vilivyoko Wilaya ya Bagamoyo na maeneo mengi ili watu wafike kujifunza.

Baadhi ya wanafunzi ambao wameshiriki katika sherehe za maadhimisho ya Uhuru kutoka shule za Bagamoyo waliishukuru TFS kwa kuwapa fursa ya kutembelea kumbukumbu mbalimbali za kihistoria zilizopo katika mji huo ikiwamo gereza la watumwa, kisima cha maji yanayoondoa matatizo na mti aina ya mbuyu wenye miaka zaidi ya 100 unaotumiwa na watu kuuzunguka kuongeza na kupunguza siku za kuishi.

# SAKATA LA BARBARA LAIBUA UJENZI UWANJA WA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya sakata la Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu ya Simba, Barbara Gonzalez, kuzuiwa kuingia kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Mshauri wa Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Crescentius Magori, amesema imefika wakati sasa klabu hiyo kufanya maamuzi magumu ya kuwa na uwanja wao wenyewe wenye uwezo wa kuchukua watazamani 30,000 ili kuepukana na vitendo vya dharau na unyanyasaji.

Magori ameandika jana kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram kuwa imefika wakati sasa wa kukataa tukio alilofanyiwa ofisa mtendaji mkuu huyo kwa vitendo na si maneno.

Magori ambaye aliwahi pia kuwa Makamu Mwenyekiti wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), pia Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, aliandika: "Pole sana Mwenyekiti wa Bodi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba kwa yaliyotokea jana, Simba ni timu kubwa sana. Tuseme 'no' (hapana) kwa vitendo.

"Tunaweza kuwa na uwanja wetu wenye uwezo wa kuchukua watazamaji 30,000 pale Bunju kama tukiamua, vitendo vya jana viwe chachu ya kuanza mradi wa Bunju leo. Rais Mohamed Dewji, Mwenyekiti wa Bodi, Mwenyekiti wa Simba, bodi nzima na Ofisa Mtendaji Mkuu Barbara, tufanye maamuzi magumu, tutaona nani atakuja kwetu kwenye mechi zetu kutupangia nani aingie uwanjani. Simba tukiamua hatushindwi." Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, aliripoti kuzuiliwa uwanjani juzi wakati wa mechi ya timu hiyo dhidi ya Yanga, mechi iliyoisha kwa suluhu.

Hata hivyo, Shirikisho la Soka nchini (TFF), lilijibu kuwa kiongozi huyo wa Simba alikuja akiwa na watoto ambao hawakuruhusiwa kuingia kwenye eneo hilo la watu maarufu kutokana na kuwa na kadi ambazo si za kwao.




Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akipiga hesabu za kumtoka beki wa Simba, Henock Inonga 'Varane', kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na timu hizo kutoka suluhu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtibwa yarejea Manungu Complex

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza baada ya misimu miwili, timu ya Mtibwa Sugar imerejea kwenye uwanja wake wa nyumbani, Manungu Complex kwa jana kucheza dhidi ya Biashara United kwenye mechi ya raundi ya nane ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Uwanja huo ulifungiwa na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), misimu miwili iliyopita baada ya kutokidhi matakwa ya kikanuni ikiwamo kuwa na mabati badala ya ukuta.

Jana uwanja huo ulionekana kuzungushiwa ukuta ingawa bado haujakamilika vizuri, huku eneo la kuchezea ('pitch'), likionekana liko vizuri, japo kuna mapungufu ya hapa na pale.

"Uwanja wetu umekamilika, tulikuwa tunanyanyasika sana, lakini ujenzi umekamilika, nadhani tukirudi nyumbani tutaanza kushinda," alisema Thobias Kifaru, msemaji wa klabu hiyo siku mbili kabla ya jana kuanza kuutumia uwanja huo.

Mtibwa Sugar ambayo imekuwa haifanyi vizuri msimu huu, na misimu ambayo ilikuwa haitumii uwanja wake, ilikuwa ikitumia viwanja kadhaa ambavyo ni CCM Gairo, Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Jamhuri Morogoro, na Mabatini Mlandizi mkoani mkoani Pwani.

Kabla ya mechi dhidi ya Biashara jana, Mtibwa ilikuwa inashika mkia ikiwa na pointi mbili, ikiwa haijashinda hata mechi moja.

# Simba hesabu kwa JKT Tanzania FA kesho

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kumalizana na Yanga kwa kutoka suluhu kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara juzi, mabingwa watetezi wa ligi hiyo jana wameingia kambini tayari kuanza kampeni ya kutetea Kombe la Azam Sports Federation maarufu FA Cup, dhidi ya JKT Tanzania kesho.

Simba na Yanga zilishindwa kutambiana katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi baada ya dakika 90 kumalizika kwa suluhu, hivyo sasa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu, watashuka tena uwanjani hapo kesho kuanza kutetea Kombe la FA dhidi ya JKT Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Simba, baada ya mchezo huo wa juzi wachezaji wote walipewa mapumziko mafupi kwenda kuonana na familia zao na jana jioni walirejea mazoezini na kwenda moja kwa moja kambini tayari kwa ajili ya mchezo huo wa kesho.

"Wachezaji wote wataingia kambini huku wale wanaoendelea kupona majeraha yao, nao wakiwamo, lengo letu ni kutetea mataji yote mawili msimu huu wa 2021/22," ilieleza taarifa ya klabu hiyo.

Baada ya mechi hiyo, Simba itaifuata Kagera Sugar mjini Bukoba tayari kwa mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa Uwanja wa Kaitaba Jumamosi wiki hii kabla ya kuelekea mjini Tabora kuvaana na KMC FC Desemba 24, mwaka huu kwenye mwendelezo wa ligi hiyo.

KMC ambayo itakuwa mwenyeji wa mchezo huo, imeamua kuhamishia mchezo huo katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora badala ya Uhuru, Dar es Salaam ambao imekuwa ikiutumia siku zote kwa mechi zake za nyumbani.

Simba ipo katika nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu Bara, ikiwa na alama 18, mbili nyuma ya Yanga inayoongoza ligi hiyo baada ya timu zote kushuka dimbani mara nane.

Kwa upande wa Kagera Sugar, yenyewe ipo nafasi ya 12 ikiwa na pointi nane baada ya kushuka dimbani mara saba kabla ya mechi ya jana usiku dhidi ya Azam FC katika Uwanja wa Chamazi, Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### LINGARD ANUKIA NEWCASTLE
NEWCASTLE imefanya mawasiliano na Manchester United juu ya uwezekano wa kumsajili kiungo wao, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28, kwenye dirisha la Januari. ***(Sun)***

### UNITED YATAKA NYOTA WANNE
MANCHESTER United wameweka orodha ya wachezaji wanne kama mshambuliaji wao mwenye umri wa miaka 34, Edinson Cavani atajiunga na Barcelona. ***(Mail)***

### LUKAKU KURUDI SERIE A
STRAIKA wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 28, atarudi Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kabla ya kustaafu soka, wakala wake amesema. ***(Tuttosport, via Goal)***

### DE VRIJ HAKIELEWEKI INTER
INTER Milan haijafanya mazungumzo yoyote ya kuongeza mkataba na mlinzi wa Uholanzi, Stefan de Vrij mwenye umri wa miaka 29, huku kukiwa na tetesi kwamba anatakiwa Tottenham na Newcastle. ***(Gazzetta dello Sport)***

### NDIDI KUMRITHI CASEMIRO
REAL Madrid imemtambua kiungo wa Leicester na Nigeria, Wilfred Ndidi mwenye umri wa miaka 25, kama ndio mbadala wa nyota wa Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 29. ***(Naija)***

### JUVE YASIKILIZIA OFA
JUVENTUS wanasikiliza ofa kwa ajili ya kiungo wao wa kimataifa wa Marekani, Weston McKennie mwenye umri wa miaka 22, nyota wa Wales, Aaron Ramsey mwenye miaka 30 na Arthur wa Brazil mwenye miaka 25, katika dirisha la Januari. ***(Gazzetta dello Sport)***

### KOZLOWSKI KUTUA BRIGHTON
KLABU ya Brighton ipo kwenye mikakati ya kuipiku Manchester City, Liverpool na AC Milan katika mbio za kuwania kumsajili nyota wa Poland mwenye umri wa miaka, 18, Kacper Kozlowski kwa dau la pauni milioni nane kutoka Pogon Szczecin. ***(Mail)***

### JANUZAJ AWANIWA BARCA
BARCELONA wanawania kumsajili kiungo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 26, Adnan Januzaj wakati mkataba wake utakapomalizika kule Real Sociedad kipindi kijacho cha majira ya joto. ***(Mail)***

### MARTIAL ATAKIWA BARCA
BARCELONA inapanga kumsajili straika wa Manchester United na Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26. ***(Sport)***

### ICARDI ATETA NA JUVE
WAKALA wa mshambuliaji wa PSG na Argentina mwenye umri wa miaka 28, Mauro Icardi ambaye ni mke wake, kwa sasa anafanya mazungumzo na Juventus ili mteja wake kujiunga na timu hiyo. ***(Fichajes)***

### PEDRI ANA FURAHA BARCA
KIUNGO wa Hispania, Pedri mwenye umri wa miaka 19, amesisitiza ana furaha kuendelea kucheza pale Barcelona licha ya kutakiwa na Manchester City. ***(Tuttosport)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ETO'O RAIS MPYA WA 'TFF' YA CAMEROON

**Tunatakiwa kuwaleta wanasoka katikati ya sera zetu, tutaanza kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanja ili kutimiza...**

**YOUNDE, Cameroon**

MCHEZAJI wa zamani wa Barcelona, Inter Milan na Chelsea, Samuel Eto'o, ndiye Rais mpya wa Shirikisho la Soka la Cameroon (Fecafoot) kwa miaka minne ijayo, baada ya kushinda uchaguzi mkuu uliofanyika Ijumaa.

Mshindi huyo mara nne wa tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa Afrika, alimshinda mpinzani wake, Seidou Mbombo Njoya, ambaye ni makamu wa nne wa Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Wagombea saba walijitokeza kwenye uchaguzi huo, lakini watano kati yao walijitoa asubuhi siku ya uchaguzi huo.

Eto'o mwenye umri wa miaka 40, ni mmoja wa wachezaji walioacha alama ya kutukuka kwenye mchezo wa soka duniani.

"Tunatakiwa kuwaleta wanasoka katikati ya sera zetu," alisema baada ya kutangazwa kwa matokeo hayo.

"Ni jukumu letu kuhakikisha wanahusika na kuujenga mchezo, wanazingatia nidhamu bora kwa ajili ya majaliwa mazuri ya baadaye."

Mchezaji huyo wa zamani wa Barcelona, Inter Milan na Chelsea, pia aliahidi kucheza angalau viwanja 10 wakati wa kipindi chake cha uongozi. "Nimezungumza na jamii ya wafanyabiashara na tutaanza kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanja ili kutimiza malengo yetu," alisema Eto'o.

Ataiongoza Fecafoot wakati nchi yake ikiwa mwenyeji wa mashindano ya Mataifa ya Afrika yanayoanza Januari na kumalizika Februari.

Miongoni mwa wagombe wa uchaguzi huo walikuwa mchezaji wa zamani wa Cameroon, Maboang Kessack na Jules Denis Onana.

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI
HOME
ROMA
1.42 | 4.92 | 6.63
SPEZIA
AWAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# IBRAHIMOVIC ATUPIA BAO LA 300 LIGI TANO ULAYA

**MILAN, Italia**

ZLATAN Ibrahimovic ameweka rekodi nyingine kwenye maisha yake ya soka baada ya kufunga bao lake la 300 katika Ligi tano kubwa Ulaya.

Mkongwe huyo wa Milan alifunga bao la kusawazisha dakika ya mwisho dhidi ya Udinese Jumamosi na pia hiyo ilikuwa mechi yake ya 450 kucheza kwenye ligi tano kubwa Ulaya.

Mabao hayo 300 ya Ibrahimovic ni jumla ya aliyofunga kwenye Ligi Kuu ya England - Premier League, Ligi Kuu ya Italia - Serie A, Ligi Kuu ya Hispania - LaLiga na Ligi Kuu ya Ufaransa - Ligue 1.

Ibrahimovic amecheza katika ligi zote nne kubwa, ni Bundesliga pekee ndio ambayo hajawahi kuichezea.

Hata hivyo, ni Cristiano Ronaldo na Lionel Messi pekee walifikisha idadi hiyo ya mabao awali kwenye karne hii ya 21, ingawa wao hawajacheza ligi zote nne kama ilivyo kwa Ibrahimovic aliyecheza hizo kati ya tano bora Ulaya.

Alijiunga na Juventus mwaka 2004 kutoka Ajax, halafu straika huyo wa Sweden akaenda kuichezea Inter Milan, Barcelona, Milan (vipindi viwili), Paris Saint-Germain na Manchester United.

Ibrahimovic sasa amefunga mabao saba kwenye Serie A msimu huu. Alifunga 15 msimu uliopita na 10 msimu wa 2019-20 baada ya kurudi hapo Milan akitokea Ligi Kuu ya Marekani (MLS), kwenye Klabu ya LA Galaxy.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 40, alifunga mabao 17 kwenye msimu mmoja kule Ligi Kuu England akiwa na United, akiwa na wastani wa kufunga bao moja kila baada ya dakika 143.

Rekodi yake bora zaidi ya kufunga mabao mengi kwa msimu mmoja ilikuja katika msimu wake wa mwisho kule PSG (2015-16) ambapo alifunga mabao 67 na kutoa asisti 13 kwa wachezaji wenzake.

Ibrahimovic alifunga mabao 38 kwenye Ligue 1. Pia alifunga mabao 30 au zaidi ya Ligi katika misimu miwili tofauti kati ya 2015-16 na 2012-13, akiwa na PSG.

Nusu ya mabao yake hayo 300 aliyafunga kwenye Ligi Kuu Italia (154), wakati Ufaransa alifunga 113.

# Arteta atoa sababu Aubameyang benchi



**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta alimuacha Pierre-Emerick Aubameyang kwenye mchezo wa Ligi Kuu England juzi Jumamosi dhidi ya Southampton kutokana na "kuvunja sheria za kinidhamu."

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, hakuwapo kwenye mazoezi Ijumaa ingawa klabu haijaweka wazi tukio alilolifanya, chanzo kimoja kutoka kwenye klabu hiyo kiliiambia ESPN ni kutokana na "sheria za COVID-19."

Akizungumza kabla ya mchezo huo, Arteta alisema: "(Aubameyang hatacheza) kwa sababu ya kuvunja sheria za kinidhamu."

"Nafikiri tumekuwa wazi kabisa kuhusu nidhamu ya timu na lazima kila mchezaji anatakiwa kufuata sheria."

Alipoulizwa kama hiyo itakuwa adhabu ya muda mrefu, Arteta aliongeza: "Inaanza leo (juzi).

"Pengine sio hali ya rahisi, au hali ambayo tunaitaka kutoka kwa nahodha wa klabu yetu." Aubameyang pia alicheza kwenye mchezo wa Machi mwaka huu wakishinda dhidi ya wapinzani wao wa London, Tottenham baada ya kuchelewa kujiunga na timu hiyo siku ya mchezo.

Arsenal katika mchezo wa juzi iliibuka na ushindi mtamu wa mabao 3-1 na kujivuta hadi nafasi ya sita kwenye msimamo ikiwa na pointi 26 baada ya kushuka dimbani mara 16.

LIVE IN PLAY

# MASHABIKI WAFURAHIA SERENGETI LAGER KUWALETEA NYOTA WA STARS

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Kampeni ya 'Nje ya Dimba na Stars' ikiendelea kuzunguka mikoani, mashabiki wameelezea kufurahishwa na kampeni hiyo inayowapa fursa ya kukutana uso kwa uso na wachezaji nyota wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Kampeni hiyo iliyozinduliwa siku kadhaa zilizopita, inalenga kuwapa nafasi mashabiki wa Taifa Stars sehemu mbalimbali hapa nchini kukutana na nyota wanaowapenda katika baa zao na pia kupata fursa ya kuwauliza maswali kuhusu maisha yao nje ya soka pamoja kupiga nao picha za ukumbusho.

Wiki iliyopita kampeni ya Nje ya Dimba ilikuwa mkoani Mbeya ambapo mashabiki wa Taifa Stars wa mkoa huo walipata fursa ya kula chakula cha jioni na baadhi ya wachezaji wa kikosi cha Stars na kupata nafasi ya kuwauliza maswali kuhusu maisha yao nje ya uwanjani na pia kupiga nao picha.

Mmoja wa mashabiki hao Lusajo Mwankenja mkazi wa Mwanjelwa, Mbeya, alisema kampeni hiyo ni moja kati ya kampeni ambazo zitawapa mashabiki fursa za kukutana na nyota wanaowapenda na kuweza kujua mengi kuhusu wachezaji hao jambo ambalo katika historia ya timu ya taifa inafanyika kwa mara ya kwanza.

"Kati ya wachezaji ambao binafsi ninawakubali sana kwenye timu ya Taifa ni Feisal Salum 'Fei Toto'. Huyu ni mmoja kati ya washambuliaji bora kabisa wenye umri mdogo kwenye timu. Sikuwahi kudhani kama ningeweza kukutana uso kwa uso na nyota huyu, naishukuru sana Bia ya Serengeti kwa kunipa fursa hii," alisema.

Shabiki mwingine Annastazia Mbengenyi, alisema wakazi wa Mbeya ni wapenda soka na timu yao ya taifa na kuongeza kuwa ilikuwa ni fursa ya kipekee kukutanishwa na nyota wa Taifa Stars ambao walizoea kuwaona kupitia vyombo vya habari, televisheni.

Akizungumza wakati kampeni hiyo jijini Mbeya, Meneja Masoko wa Kanda za Juu Kusini wa Serengeti Breweries Limited (SBL), Denis Tairo, alisema Bia ya Serengeti Lager ikiwa kama shabiki mkuu wa Taifa Stars, inajivunia kuwaletea mashabiki wa timu hiyo jijini Mbeya nyota wanaowapenda na kuwapa nafasi ya kuzungumza nao na hivyo kuwafahamu kwa undani zaidi.

"Shabiki mkuu na mdhamini wa timu yetu ya Taifa, Taifa Stars, Bia ya Serengeti Lager amewakutanisha mashabiki wa hapa Mbeya uso kwa uso na nyota ambao mara nyingi wamekuwa wakiwaona uwanjani. Hii ni fursa pekee ya mashabiki kujua maisha ya nyota wao nje ya uwanjani," alisema.




Mchezaji wa Taifa Stars, Bakari Mwamnyeto, akizungumza wakati baadhi ya wachezaji wa timu hiyo walipotembelea jijini Mbeya hivi karibuni, ikiwa ni sehemu ya Kampeni ya 'Nje ya Dimba na Stars' inayoendeshwa na Bia ya Serengeti Lager. **MPIGAPICHA WETU**

Denis alisema kampeni hiyo ya nchi nzima itahusisha wachezaji wa Taifa Stars ambapo watatembelea mikoa ya Mbeya, Mwanza na Arusha na kukutana na mashabiki wao kupitia matukio kama pati za mwisho wa mwezi 'Nje ya Dimba na Stars'. Kwenye matukio kama hayo mashabiki wataweza pia kujishindia zawadi mbalimbali na ofa za bia yao pendwa ya Serengeti Lager.

"Wachezaji watakuwa kwenye baa mbalimbali na wakati wateja wetu wa bia ya Serengeti Lager wakiendelea kuburudika na bia yao pendwa iliyotengenezwa kwa kimea kwa asilimia 100 na isiyoongezwa sukari, watapata nafasi ya kuwauliza maswali, kupiga picha na kupata sahihi zao," alisema.


SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 13 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 4370 | Jezero vs Zeta Golubovci | 2.46 | 2.99 | 2.79 |
| 15:20 | 2419 | Al Jabalain vs AL Kawkab | 1.66 | 3.47 | 4.81 |
| 16:00 | 1146 | Sirens vs Gudja United | 1.58 | 4.05 | 4.53 |
| 16:00 | 3177 | FC Koln II vs FC Schalke 04 II | 1.63 | 3.96 | 4.25 |
| 16:30 | 4039 | Persiraja Banda vs PSM Makassar | 6.38 | 4.45 | 1.39 |
| 16:30 | 5950 | Bologna Youth vs Empoli Youth | 4.23 | 4.14 | 1.61 |
| 17:00 | 2862 | Excelsior Virton U21 vs Oostende U21 | 3.97 | 4.16 | 1.65 |
| 17:00 | 3506 | Hyderabad FC vs Northeast United FC | 2.40 | 3.27 | 2.64 |
| 17:00 | 3623 | Fiorentina Youth vs Torino Youth | 1.85 | 3.56 | 3.61 |
| 17:25 | 4411 | Al Khaleej Club vs Hajer Club | 2.04 | 2.99 | 3.62 |
| 17:30 | 2510 | Ludogorets Razgrad vs Pirin Blagoevgrad | 1.16 | 6.58 | 11.60 |
| 17:45 | 2541 | Metalac vs Partizan | 14.50 | 6.19 | 1.15 |
| 18:00 | 2654 | Sivasspor vs Galatasaray | 2.86 | 3.21 | 2.42 |
| 18:00 | 4170 | Portimonense U23 vs Benfica U23 | 4.05 | 3.76 | 1.70 |
| 18:20 | 5740 | Al Wehda vs Jeddah Club | 1.59 | 3.58 | 5.23 |
| 18:45 | 1140 | Teuta Durres vs Kukesi | 2.50 | 3.12 | 2.64 |
| 19:00 | 1175 | Sochi vs Spartak Moscow | 2.00 | 3.43 | 3.48 |
| 19:00 | 1235 | Omonia Nicosia vs AEK Larnaca | 2.34 | 3.21 | 3.01 |
| 20:00 | 1562 | Anorthosis Famagusta vs Doxa Katokopia | 1.65 | 3.68 | 5.18 |
| 20:00 | 1869 | Hapoel Raanana vs Sectzya Nes Ziona | 2.57 | 3.07 | 2.82 |
| 20:00 | 2726 | Red Star Belgrade vs Radnik Surduluca | 1.07 | 8.64 | 22.07 |
| 20:00 | 2941 | Hapoel Afula vs El Fahem | 2.73 | 3.17 | 2.58 |
| 20:00 | 3915 | Hapoel Rishon Lezion vs Hapoel Ramat Gan | 2.54 | 3.29 | 2.69 |
| 20:00 | 4035 | Warta Poznan vs Slask Wroclaw | 2.84 | 3.13 | 2.33 |
| 20:30 | 3302 | Gaziantep BB vs Fenerbahce | 3.21 | 3.40 | 2.13 |
| 21:00 | 2578 | CF Estrela vs Casa Pia Atletico | 2.98 | 3.28 | 2.25 |
| 21:00 | 5904 | Wehen vs Hallescher | 1.95 | 3.38 | 3.68 |
| 21:15 | 1060 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Hadera | 1.40 | 4.24 | 6.74 |
| 21:30 | 1090 | Mouscron U21 vs Lierse SK | 1.74 | 3.95 | 3.66 |
| 21:30 | 2431 | AS Eupen U21 vs Lommel U21 | 1.22 | 6.17 | 8.68 |
| 21:30 | 4149 | Waasland Beveren U21 vs Kortrijk U21 | 1.72 | 3.85 | 3.85 |
| 21:30 | 5328 | Club Nxt vs Anderlecht U21 | 1.71 | 4.05 | 3.71 |
| 21:30 | 5763 | Dinamo Bucuresti vs Chindia Targoviste | 2.65 | 3.00 | 2.70 |
| 21:45 | 3805 | Partizani Tirana vs Din. Tirana | 1.59 | 3.41 | 5.57 |
| 21:45 | 5122 | Maccabi Haifa vs Beitar Jerusalem | 1.31 | 4.81 | 7.88 |
| 22:00 | 2302 | Hull City U23 vs Peterborough United Reserve | 2.35 | 3.75 | 2.45 |
| 22:00 | 2615 | Jeugd Rfc Seraing United U21 vs Beerschot Wilrijk U21 | 3.95 | 3.95 | 1.69 |
| 22:00 | 4164 | Wigan U23 vs Crewe U23 | 1.44 | 4.52 | 5.39 |
| 22:00 | 5617 | Union Saint Gilloise U21 vs RWD Molenbeek U21 | 1.90 | 3.80 | 3.23 |
| 22:00 | 5656 | Kmsk Deinze U21 vs Westerlo U21 | 2.50 | 3.60 | 2.60 |
| 22:45 | 1686 | Roma vs Spezia | 1.42 | 4.92 | 6.63 |
| 22:45 | 1803 | Sheffield Utd vs QPR | 1.81 | 3.59 | 4.03 |
| 22:45 | 2539 | Sedan vs Red Star | 3.28 | 3.08 | 2.19 |
| 22:45 | 4162 | Toulouse vs Rodez Aveyron | 1.57 | 3.73 | 5.70 |
| 23:00 | 1405 | Esperanca De Lagos vs Olhanense | 2.79 | 3.37 | 2.24 |
| 23:00 | 1490 | Virtus Entella vs AC Reggiana | 2.63 | 3.17 | 2.68 |
| 23:00 | 2142 | Mirandes vs Real Sociedad B | 2.14 | 3.15 | 3.40 |
| 23:00 | 4851 | Cadiz CF vs Granada | 2.49 | 3.09 | 2.99 |
| 23:00 | 5668 | Barracas Central vs Almirante Brown | 2.08 | 3.23 | 3.23 |
| 23:15 | 4283 | FC Arouca vs FC Vizela | 2.21 | 3.24 | 3.19 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatui Desemba 13, 2021

Nipashe





UKURASA 21

## Eto'o rais mpya wa 'TFF' ya Cameroon

NGOME...



# HAIKUWA RAHISI

●●●Nabi aivulia kofia Simba, Pablo afunguka ufundi kutawala, asema...

Winga wa Simba, Mghana Bernard Morrison, akijiandaa kuipenya ngome ya ulinzi ya Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga Nasreddine Nabi amekisifu kikosi cha Simba na kusema kimeonekana kuimarika tofauti na alivyokiona kwa siku za karibuni, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema bado anaendelea kukiimarisha kikosi chake na ana imani kwenye mechi ya mzunguko wa pili kitakuwa bora zaidi.

Wakizungumza baada ya kumalizika mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, makocha hayo wameelezea kila mmoja kuridhishwa na suluhu ambayo imepatikana, huku wakiuelezea mchezo huo kiufundi zaidi.

"Mchezo ulikuwa mzuri, ulitawaliwa na mbinu nyingi na ndio maana hakukuwa na nafasi nyingi, Yanga tulicheza vizuri kipindi cha kwanza kwa kukosa nafasi kadhaa za kufunga, Simba ikacheza vizuri kipindi cha pili na kutengeneza nafasi ambayo Diarra (Djigui) aliokoa. Wapinzani wetu wameimarika na tulichofanya ni kuwazuia wasipate nafasi ya kufunga, alisema raia huyo wa Tunisia.

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo yeye amesema bado ana safari ndefu ya kuendelea kuijenga timu, na ana imani kama wakikutana na Yanga kwenye mechi inayofuata ya mzunguko wa pili, basi watakuwa bora zaidi ya walivyocheza leo.

"Bado tuna safari ya kuendelea kujenga timu, nina imani tukikutana tena mchezo ujao tutakuwa bora zaidi, lakini ninajivunia sana wachezaji wangu. Kipindi cha pili tulicheza vizuri zaidi, tulikuwa na nafasi kubwa ya kushinda. Tulikuwa tuna ari na malengo zaidi ya wapinzania wetu, lakini hatukutumia nafasi, naamini tutaendelea kuimarisha," alisema raia huyo wa Hispania ambaye aliiongoza timu hiyo kwa mara ya kwanza kwenye mchezo wa watani wa jadi 'dabi'.

Straika wa Simba, Meddie Kagere alisema Simba na Yanga ni timu kubwa na 'dabi' ya Tanzania ni bora kwa sasa, hivyo karibu wachezaji wote walionekana kuwa na utayari wa mechi hiyo.

"Tumekosa nafasi za kufunga mabao, lakini hili linatokea kwenye mechi kama hizi kubwa, unaweza usipate kabisa nafasi, ukazipata na ukashindwa kuzitumia," alisema Kagere ambaye kwa sasa ni mzoefu kwenye mechi za watani nchini.

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alikiri kuwa mechi ilikuwa ngumu na anachoona kila timu ilijihami kwenye dakika za mwanzo isiruhusu bao la mapema, huku kipindi cha pili kila timu ikishambulia kwa tahadhari.

"Kila timu imepata pointi moja, siyo mbaya kwa jinsi tulivyocheza sisi na Simba, ni halali kila mmoja kupata pointi moja, wao walitupania na sisi tuliwapania," alisema.

Baada ya suluhu hiyo, timu hizo zimeungana na Mbeya City kucheza mechi nane mfululizo za Ligi Kuu bila kupoteza mechi yoyote.

Yanga inaendelea kuongoza ligi ikiwa na pointi 20, huku Simba ikijichimbia nafasi ya pili kwa pointi 17.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042